

# MUHURI WA SITA



Na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa muda kidogo.

<sup>2</sup> Bwana, tunakusanyika tena kwa ajili ya ibada. Na tunaukumbuka ule wakati, katika zile siku za mwanzoni, wakati watu wote walipopanda kuja kule Shilo kwa ajili ya baraka za Bwana. Na sasa, usiku wa leo, tumekusanyika hapa kulisikia Neno Lako. Nasi kama tulivyokuwa tukisoma katika sehemu hii ya Maandiko, ya kwamba Mwana-Kondoo alikuwa ndiye tu ambaye angeliweza kufungua ile Mihuri, ama kuiachilia. Nasi tunaomba ya kwamba usiku wa leo, kwa kuwa tuna wajibu wa kujifunza Muhuri huu mkuu wa Sita, tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba Mwana-Kondoo ataufungua kwetu usiku wa leo. Kwamba, tuko hapa ili tuufahamu. Na wakati hakuna mtu duniani, au Mbinguni, aliyekuwa anastahili, Mwana-Kondoo tu ndiye aliyeonekana anastahili. Kwa hiyo Yeye anayetosheleza katika yote na aje na kutufungulia Muhuri huu usiku wa leo, ili tuweze kuangalia tu ng'ambo ya pazia la wakati. Ingetusaidia, tunaamini, Baba; siku hii kuu, yenye giza, na iliyojaa dhambi tunayoishi; ingetusaidia na kutupa ujasiri. Tunaamini sasa ya kwamba tutapata neema machoni Pako. Tunajikabidhi, pamoja na Neno, Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mnaweza kuketi.

<sup>3</sup> Habari za jioni, wapendwa. Ni majaliwa kuwa hapa tena usiku wa leo, kuwa katika utumishi wa Bwana. Nilikuwa tu nimechelewa kidogo. Nilienda tu kuninii. . . kwenye dharura, ya mtu anayekufa, ya mshiriki wa kanisa hili; mama yake ni mshiriki, ama yeye anahudhuria hapa. Nao walisema ya kwamba huyo kijana alikuwa akifa wakati huo huo. Kwa hiyo ni—nikashuka nikaenda kuona ki—kivuli tu cha mtu aliyelala kitandani anakufa, mtu wa umri kama wangu. Na katika tu kufumba na kufumbua, nilimwona mtu akisimama kwa miguu yake, akimpa Bwana sifa. Na kwa hiyo, Mungu, kama tutakuwa tayari kukiri dhambi zetu na kufanya lile lililo jema, kuomba rehema, kumwita Yeye, Mungu yuko tayari na anangojea kutupa jambo hilo.

<sup>4</sup> Na, sasa, ninajua kuna joto hapa ndani usiku wa leo. Na—na ni ninii. . . La, nadhani joto limezuiwa kabisa. Nasi—nasi tu ninii. . .

<sup>5</sup> Nilitambua jana usiku, ama leo, hii ni siku yangu ya saba kwenye chumba kisicho na taa, hasa taa za umeme, mnaona; nikisoma, na kuomba kwamba Mungu afungue Mihuri hii.

<sup>6</sup> Na kulikuwa na wengi sana ambao wameandika, katika kundi lile la wanaouliza ja-. . . ama maswali jana usiku,

yalikuwa, kwa namna moja ama nyingine, zaidi sana si maswali. Walitaka kuwa na ibada ya kuponya, hata hivyo; walitaka kukaa siku moja zaidi, ili wawe na . . . wawe na ibada ya uponyaji Jumatatu. Kwa hiyo ni—ni—ningeweza, ningeweza, kwa kweli ningeweza kufanya hivyo kama hayo yangelikuwa ndiyo mapenzi ya watu ya kwamba wangepanya jambo hilo. Mnaweza kulifikiria na kuniambia, iwapo tu kama mnataka tu kukaa na kuwaombea wagonjwa.

<sup>7</sup> Kwa sababu, nimeupangia wakati huu wote, kabisa, kwa ajili ya Mihuri hii, na kujitenga tu kwa ajili ya Mihuri hii.

<sup>8</sup> Kwa hiyo mnaweza kulifikira jambo hilo, na kuliombea, na halafu mniulishe. Nami nitaninii, Bwana akipenda, ninaweza. Mkutano wangu ufuatao utakuwa ni huko Albuquerque, New Mexico, na hiyo itakuwa zimebakia si—siku chache. Nami sina budi kurudi nyumbani kwa ajili ya shughuli fulani, ya kuandaa mkutano mwingine huko Arizona. Na kwa hiyo, basi, kama ni mapenzi ya Bwana! Ombeeni jambo hilo, nami nitafanya vivyo hivyo, ndipo tutajua habari zake zaidi baadaye.

<sup>9</sup> Sasa hivi tu ndiyo nimeona. Sasa ninaona . . . Ukianza kuzungumza juu ya magonjwa, huo unakuja, unaona. Ninamwona bibi huyu aliyeketi papa hapa. Kama kitu fulani hakitamsaidia, hatakaa hapa ila kwa muda mfupi. Kwa hiyo, basi, unaona, tu—tunaomba tu kwamba Mungu atamsaidia. Hilo ndilo lililokuleta hapa, unatoka mbali sana. Kwa hiyo, unaona, Ro—Roho Mtakatifu anajua tu kila kitu, unaona. Kwa hiyo Bwana . . .

<sup>10</sup> Lakini, unaona, nimejaribu kutenga wakati huu kwa ajili ya Mihuri hii, sababu tuliuweka kwa ajili ya hiyo, unaona. Lakini kama kuna ninii . . .

<sup>11</sup> Ni wangapi hapa walio wagonjwa, hata hivyo, ambao wamekuja kuombewa? Hebu tuone mikono yenu, kote kote, kila mahali. Loo! jamani! A-ha! Vema, ni wangapi wangepifikiria ya kwamba jambo hilo lingekuwa ni sawa, mapenzi ya Bwana, kukaa na kuendesha jambo hili, kuchukua Jumatatu usiku, kuwaombea tu wagonjwa, kufanya ibada ya uponyaji Jumatatu usiku? Je! mngetaka kufanya jambo hilo? Mngeweza kulifanya? Vema, Bwana akipenda, tutafanya hivyo basi. Mnaona? Tuta—tufanya ibada ya uponyaji kwa ajili ya wagonjwa, Jumatano, ama Jumapili usiku, ama . . . Jumatatu usiku, na kuwaombea wagonjwa.

<sup>12</sup> Sasa, natumaini hilo halitavunja utaratibu wa kundi lile nitakalorudi nalo, kurudi Arizona. Ndugu Norman, je! yeye yuko hapa mahali fulani? Je! hilo linavunja utaratibu wa mpango wenu, Ndugu Norman, cho chote? [Ndugu Gene Norman anasema, “La.”—Mh.] Ndugu Fred na wengine wenu, hilo ni sawa? [Hao wengine wanasema, “Sawa.”] Unaona? Hilo ni sawa. Vema.

13 Halafu, Bwana akipenda, Jumatatu usiku tutawaombea wagonjwa, usiku mmoja tu uliotengwa kwa ajili ya jambo hilo, kabisa, kuwaombea tu wagonjwa. Sasa, haitakuwa ni jambo la Mihuri tena. Kama Bwana ataifungua tu Mihuri hii, basi tutawaombea wagonjwa, Jumatatu usiku.

14 Sasa, loo! nimekuwa kweli nikifurahia hili, vizuri sana, jambo la kumtumikia Bwana chini ya Hii! Je! mmefurahia jambo Hili, kufunguliwa kwa ile Mihuri? [Kusanyiko linasema, "Amina!"—Mh.]

15 Sasa, sasa tunazungumza kutoka kwenye Muhuri wa Tano ama . . . Muhuri wa sita, hasa. Na huo unaanzia sasa kutoka ki—kifungu cha 12 cha mlango wa 6, mpaka cha 17. Ni mmoja wa ile Mihuri iliyo mirefu sana. Kuna pia mambo mengi sana yanayotukia hapa. Na sasa ninii . . .

16 Nirudie kidogo ya usiku wa jana, kwa namna fulani kurudi nyuma kidogo, kila wakati.

17 Na, kwa kuongezea, na—nataka kusema jambo fulani, pia. Nilipata, kwenye kile kijisanduku, mambo manne ama matano yaliyo muhimu sana kwangu. Niliambiwa ya kwamba . . . Na kwa kweli ninataka kuomba msamaha. Je! tepu zinaendelea kurekodi? Tepu zinarekodi? Ninataka kuwaomba msamaha rafiki zangu wahudumu na kwenu ninyi watu hapa. Wao wanasema, juzijuzi usiku nilipokuwa nikinena habari za—za Eliya, kwenye ile saa ambapo wao walikuwa . . . Yeye alidhani alikuwa ndiye pekee yake atayeenda kwenye Unyakuo, ama ndiye pekee atakayeokolewa. Ni—nilisema mia saba badala ya elfu saba. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko, "Ndio."—Mh.] Vema, kweli samahani kwa jambo hilo, jamani. Ni—ni—nililijua jambo hilo vizuri sana. Ilikuwa tu ni kuteleza kwa ulimi, maana nilijua ilikuwa ni elfu saba. Sikulisema tu sawa. Mimi . . . Nami na—nawashukuru. Na hilo linamaanisha ya kwamba . . . Ninashukuru kwamba ninyi mmekaa macho kwa yale ninayosema. Nanyi mnaona, basi, hiyo . . . Maana, ni, ni—ninii elfu saba.

18 Nilipata hoja mbili ama tatu nilizoandikiwa juu ya jambo hilo, ambazo zilisema, "Ndugu Branham, nadhani ulikosea." Ikasema, "Je! hao si walikuwa ni elfu saba badala ya mia saba?"

19 Nikawaza, "Hakika sikusema mia saba." Mnaona? Hilo, na halafu mimi . . . Billy . . .

20 Na halafu mimi, muda si muda unajua, nikachukua kijikaratasi kingine. Kilisema, "Ndugu Branham, ulininii . . . Ninaamini ulisema mia saba."

21 Na mtu mmoja akasema, "Ndugu Branham, je! hilo lilikuwa ni o—ono la kiroho ya kwamba—kwamba kutakuwako tu na mfano, nawe unafananisha na wale nini saba . . .?" Inawafanya watu kuwa na wasiwasi unapoanza kuwazia mambo haya, unaona. Na imetosha, hiyo, kunitia wasiwasi.

22 Jambo fulani lilitukia leo wakati Muhuri huu ulipofunuliwa, hivi kwamba ilinibidi nitoke nje kabisa kwenda zangu uwanjani, kutembea-tembea tu, huko uwanjani kidogo. Hiyo ni kweli. Karibu tu nishindwe kupumua. Unaona? Kwa hiyo unazungumzia, kiherehere kikubwa sana? Loo! jamani! Unaona?

23 Jambo lingine, unaona, mnashikilia moja kwa moja yale nisemayo. Na Mungu atanitaka niwajibike kwa yale ninayowaambia. Mnaona? Na kwa hiyo mimi—mimi sina budi kuwa na hakika yakini kama hakika ipaswavyo kuwa kabisa, unaona, juu ya mambo haya, kwa maana huu ni wakati mu—muhimu sana tunaishi. Naam.

24 Nilikuwa nifikiria juu ya ibada ya uponyaji kwa ajili ya Jumatatu usiku. Hiyo ingekuingilia, Ndugu Neville mahali po pote? [Ndugu Neville anasema, “Hata kidogo. Nitakuwa papa hapa.”—Mh.] Hilo ni sawa.

25 Maskini Ndugu mpendwa Neville! Nawaambieni, wao wali—walimpata tu mmoja, nafikiri, harafu wakapoteza mfano wake. Ni . . . Kweli amekuwa rafiki msiri wangu ha—hasa na mwenzangu, nawaambieni.

26 Maskani imejengwa sasa, na ina vyumba vya shule ya Jumapili na kila kitu tayari, katika utaratibu hapa. Na baadhi yenu ninyi watu mlio karibu na hapa, karibu na Jeffersonville, mnaotaka kuja kanisani, mna mahali pazuri, na mahali pa kuhudhuria, vyumba vya shule ya Jumapili.

27 Mwalimu mzuri, na Ndugu Neville hapa, kwa ajili ya darasa la watu wazima, na mchungaji wa kweli. Sisemi hilo kwa ajili ya kumpa shada la maua, lakini ni afadhali nimpe waridi dogo sasa kuliko shada zima baada ya yeye kuaga dunia. Na Ndugu—Ndugu Neville, nilimjua tangu nilipokuwa mvulana mdogo tu. Sasa, yeye hajabadilika hata kidogo. Yeye angali ni Orman Neville, kama tu alivyokuwa sikuzote.

28 Ninakumbuka nilipomtembelea. Hata alikuwa na neema ya kutosha kuniomba niingie mimbarani mwake wakati alipokuwa mhubiri wa Kimethodisti hapa mjini. Nasi tulikuwa na kusanyiko zuri kule Clarksville, ile . . . Nafikiri hiyo panaitwa Howard Park, kanisa la Kimethodisti la Barabara Kuu ya Harisson. Nafikiri ndiko hapana shaka alikokupata, huko, Dada Neville. Huko, sababu huyo dada alikuwa mfua- . . .

29 Nilirudi, nami nikaliambia kanisa hapa, nilisema, “Huyo alikuwa . . . Huyo ni mmoja wa watu walio wazuri sana! Na moja ya siku hizi nitambatiza katika Jina la Bwana Yesu Kristo.” Likatukia.

30 Huyu hapa. Na sasa yeye ni rafiki yangu mpendwa, yuko bega kwa bega pamoja nami. Na ni mtu muungwana sana, mtu anayeheshimika! Daima amesimama pamoja nami namna kama tu . . . amesimama karibu sana alivyoweza kusimama. Lo lote

nisemalo, yeye huniunga tu mkono na kuambatana nami moja kwa moja. Hata wakati alipokuja kwa mara yake ya kwanza, yeye hakuufahamu Ujumbe wakati huo, lakini aliuamini Huo na kudumu Nao. Huo ni uaminifu, huko ni kuheshimu, kwa ndugu kama huyo. Siwezi kusema ya kutosha juu yake. Na sasa Bwana na ambariki. Vema.

<sup>31</sup> Sasa marudio mafupi ya jana jioni, katika kule kuvunjwa kwa Muhuri wa Tano. Hatutarudi moja kwa moja huko nyuma usiku wa leo, tutarudi tu nyuma kutosha kuupata Mu—Muhuri wa Tano.

<sup>32</sup> Sasa, tunaona ya kwamba kulikuwako na mpinga-Kristo aliyepanda farasi, naye akamalizikia, katika nguvu tatu. Zote zikaingia kwenye nguvu moja, ndipo akapanda farasi wa kijivujivu, “Mauti,” akaingia kuzimu, akaenda upotevuni, mahali alikotoka. Halafu tunaona wakati. . .

<sup>33</sup> Maandiko yanasema, “Adui anapoingia kama mafuriko, Roho wa Mungu humwinulia beramu.” Nasi tuliona hilo limethibitishwa kikamilifu katika Neno jana usiku, kwa maana kulikuwako na Wenye Uhai wanne ambao—ambao walimkabili—waliomkabili mpanda farasi huyu zile mara nne alizopanda farasi.

<sup>34</sup> Naye alipanda farasi wa tofauti kila wakati, farasi mweupe, na halafu farasi mwekundu, na farasi mweusi, na halafu farasi wa kijivujivu. Nasi tuliona, rangi zile, na kwamba zilikuwa ni nini na zilifanya nini. Kisha tukawachukua moja kwa moja tukawarudisha kwenye nyakati za makanisa, na hivyo ndivyo walivyofanya kabisa, kikamilifu kabisa.

<sup>35</sup> Kwa hiyo, unaona, wakati Neno la Mungu linapoungana pamoja, hilo linamaanisha kwamba ni sahihi, unaona. Naam. Ninaamini, kitu cho chote kinachoshikamana na Neno la Mungu daima ni “amina.” Unaona?

<sup>36</sup> Sasa, kama vile mtu fulani alivyosema walipata ono, na akasema ya kwamba lilikuwa ni ono. Loo! wanajua Bwana alilionyesha, ati kwa sababu lilikuja kwa nguvu nyingi. Vema, hilo ono huenda lilikuwa ni sawa. Lakini iwapo haliambatani na Neno na ni kinyume na Neno, si la kweli. Unaona?

<sup>37</sup> Sasa, sasa huenda wakawapo, baadhi ya ndugu wa Kimormoni ama dada. Na huenda kukawa na wengine wanaopata kanda hizi, sasa. Na sitaki kusema ya kwamba. . . Baadhi ya watu wazuri sana ambao wewe na mimi tunataka kukutana nao, wangukuwa—wangukuwa ni watu wa Mormoni; watu walio wazuri sana. Na halafu nabii wao—wao, Joseph Smith, ambaye Wamethodisti walimwua hapa Illinois, walipokuwa safarini wakija huku. Na kwa hiyo basi huyo—mtu huyo mzuri, na lile ono, sishuku kamwe kwamba yeye aliona ono. Ninaamini yeye alikuwa ni mtu mwaminifu. Lakini ono aliloona lilikuwa ni kinyume cha Maandiko. Unaona? Kwa

hiyo, iliwabidi wajifanyie Biblia ya Mormoni, ku—kupitisha hilo. Unaona?

<sup>38</sup> *Hili* hapa ndilo Lenyewe, kwangu mimi. Hili Ndilo. Hiyo ndiyo sababu, Neno pekee. Hilo Ndilo. Unaona?

<sup>39</sup> Wakati mmoja, m—m—mhudumu mmoja alikuja hapa kutoka ng'ambo, naye. . . Nami nilimwona ametoka akiwa na—na. . . akizungukazunguka katika gari, jambo ambalo si ninii. . . akiwa na ma—mama mmoja. Nao wakaja mkutanoni. Nami nikagundua kwamba, walikuwa wamesafiri kwenye gari siku mbili ama tatu, wakiwa mwanamume na mwanamke peke yao, kwenye mkutano, kuja mkutanoni, pamoja. Na huyo mwanamke alikuwa ameolewa, mara tatu ama nne mbalimbali.

<sup>40</sup> Ndipo mhudumu huyu akaja kwenye ukumbi wa hoteli niliyokuwa, naye akanikimbilia na kunipa mkono. Nami nikampa mkono, nikasimama na nilikuwa nikizungumza naye. Nikamwuliza, nikasema, “Utakapopata nafasi, je! ningeweza kuongea kidogo na wewe chumbani mwangu?”

Akasema, “Ndiyo, Ndugu Branham.”

<sup>41</sup> Nikampeleka chumbani. Ndipo nikamwambia huyo mhudumu, nikasema, “Kasisi, bwana, wewe ni mgeni katika nchi hii.” Nikasema, “Lakini mama huyu ana sifa mbaya sana.” Nikasema, “Hivi. . . Nawe umetoka huko mbali mahali *fulani*, ukaja mahali *fulani* hapa?”

Kasema, “Naam, bwana.”

<sup>42</sup> Baadaye nikasema, “Je! huogopi ya kwamba jambo hilo kwa namna fulani litaninii. . . Sikutilii shaka, lakini je! wewe hudhani kwamba itakuumbua sifa yako kama mhudumu? Je! hudhani kwamba inatupasa kutoa mfano mzuri zaidi ya huo?”

Naye akasema, “Loo! mama huyu ni mtakatifu.”

<sup>43</sup> Nikasema, “Si—sishuku jambo hilo.” Lakini nikasema, “Lakini, ndugu, jambo lenyewe ni kwamba, si kila mtu anayemwangalia yeye ni mtakatifu, unaona, ambaye anaangalia unayofanya.” Nami nikasema, “Nafikiri ni afadhali uwe mwangalifu. Hilo ni kati ya ndugu mmoja kwa mwingine.” Kisha akasema. . . Nikasema, “Mama huyo amekwisha olewa mara nne ama tano sasa.”

Naye akasema, “Ndiyo, ninajua hilo.” Kasema, “Unajua, ni—ni— . . .”

<sup>44</sup> Nikasema, “Hufundishi jambo hilo huko kanisani kwako huko nyumbani, sivyo, namna hiyo?”

<sup>45</sup> Kwa hiyo kasema, “La. Lakini,” kasema, “unajua, nilipata ono la jambo hilo, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Vema, hilo ni sawa.” Nikasema. . .

46 Yeye akasema, “Unajali?” Kasema, “Akaongeza, “Ninaamini ningeweza kukusahihisha kidogo kwenye fundisho lako juu ya jambo hilo.”

47 Nami nikasema, “Vema.” Naye. . . Nikasema, “Ningefurahi kujua jambo hilo, bwana.”

48 Naye akasema, “Vema,” kasema, “unajua, katika ono hili,” akasema, “nilikuwa nimelala.”

Nami nikasema, “Naam.” Niliona, kumbe, ilikuwa ni ndoto. Unaona?

49 Ndipo akasema, “M—mke wangu,” kasema, “alikuwa anaishi na mwanamume mwingine,” kisha kasema, “na kunidanganya.” Tena akasema, “Ndipo akanijia, na akaniambia, ‘Loo!, mpenzi, nisamehe, nisamehe!’ Kasema, ‘Na—na—na—nasikitika nilifanya jambo hilo. Nitakuwa mwaminifu tangu sasa na kuendelea.” Kasema, “Bila shaka, nilimpenda sana, ninamsamehe tu, kasema, ‘Sawa.’” Na kasema, “Halafu. . .”

50 Kisha akasema, “Unajua nini? Ndipo nikapata tafsiri ya ono hili.” Kasema, “Huyo alikuwa ndiye yule mwanamke huyo.” Kasema, “Hakika, yeye ameolewa, na—na kadhalika, na mara hizi zote.” Ndipo akasema, ya kwamba, “Ni sawa kwake kuolewa, kwa sababu Bwana alimpenda sana. Anaweza kuolewa mara nyingi atakavyo, kadiri. . .”

51 Nikasema, “Ono lako lilikuwa ni zuri mno, lakini lilikuwa liko mbali sana na Njia hii ya kale hapa.” Nikasema, “Hilo—hilo ni kosa, unaona. Hupaswi kufanya jambo hilo.” Kwa hiyo hilo. . . Unaona?

52 Lakini unapoona Andiko, likiumana na Andiko, ikifanya mfululizo usiokatika yanapoungana. Maandiko, ambapo Hili linaishia hapa, Hili lingine upande huu linakuja na kuungana nalo, na kuchora picha yote nzima.

53 Ni kama kujaza mchezo wa mafumbo ya maneno, kama hivyo. Unatafuta kipande kinachoenea vizuri hapo. Hakuna kitu kingine kinachoweza kuenea. Ndipo unatengeneza hiyo picha.

54 Na kuna Mmoja tu anayeweza kufanya jambo hilo, huyo ni Mwana-Kondoo, na kwa hiyo tunamtegemea Yeye.

55 Lakini tunaona ya kwamba wakati hawa, mpanda farasi huyu, ilikuwa ni mpanda farasi mmoja aliyewapanda farasi hawa. Na ndipo tulipomfuatilia moja kwa moja, tukaona aliyofanya na kila kitu, na kuona, kule nyuma kwenye nyakati za kanisa hivyo ndivyo alivyofanya hasa.

56 Ndipo wakati yeye alipotoka amepanda mnyama fulani na kufanya jambo fulani, tunaona ya kwamba kulikuwa na mmoja aliyetumwa kushindana na yale aliyofanya.

57 Kulikuwa na mmoja aliyetumwa kwa ajili ya wakati wa kwanza, wa mwana-kondoo. . . wa simba. Huyo alikuwa ni Neno, bila shaka, Kristo.

58 Wa pili alikuwa ni ndama, katika ule wakati wa wakati wa giza, wakati—wakati ninii—kanisa lilipokuwa limeunda madhehebu na kukubali mafundisho ya sharti badala ya Neno.

59 Basi kumbukeni, jambo lote limewekwa msingi juu ya mambo mawili: moja, mpinga-Kristo; na hilo lingine, juu ya Kristo.

60 Lingali ni jambo lile lile leo. Hakuna Wakristo nusu. Hakuna mlevi-asiye mlevi; hakuna ndege weusi-weupe; la, la; hakuna wenye dhambi-watakatifu. La. Aidha wewe ni mwenye dhambi au ni mtakatifu. Unaona? Hakuna tu wa katikati. Aidha umezaliwa mara ya pili ama hukuzaliwa mara ya pili. Aidha umejazwa na Roho Mtakatifu ama hujajazwa na Roho Mtakatifu. Haidhuru ulikuwa na miamsho mingapi, kama hujajazwa na Roho Mtakatifu, hujajazwa Naye. Unaona? Na kama umezaliwa Naye, maisha yako yanaonyesha jambo hilo, yanaambatana Naye. Unaona? Hakuna mtu anayepaswa kumwambia mtu ye yote juu yake. Wao wanaliona, unaona, maana ni Muhuri.

61 Sasa, na tunawaona hao wanyama, jinsi walivyopandwa kila wakati. Mmoja aliondoka akaenda katika huduma yake, katika nguvu za kisiasa, akiunganisha nguvu za kidini na—na nguvu za kisiasa, pamoja. Tunaona ya kwamba, Mungu alituma nguvu Zake kushindana naye. Tunarudi moja kwa moja na kuona jinsi wakati wa kanisa ulivyokuwa, na tukaangalia nyuma; na hilo hapo hapo, vivyo hivyo tu kabisa.

62 Ndipo tunaona, wakati mwingine ukatokea, naye adui akamtuma mpinga-Kristo chini ya jina la dini, chini ya Jina la Kristo, chini ya jina la Kanisa. Naam, bwana. Hata, alitoka akaenda zake chini ya jina la Kanisa. “Hilo lilikuwa ni lile Kanisa halisi,” alisema. Unaona?

Mpinga Kristo si Urusi. Mpinga-Kristo si Urusi.

63 Mpinga-Kristo anafanana sana na Ukristo halisi, hata, Biblia ilisema, “Ingedanganya kila kitu ambacho hakikuchaguliwa tangu zamani.” Hilo ni kweli. Biblia ilisema ya kwamba, “Katika siku za mwisho, kila kitu ambacho hakikuchaguliwa tangu zamani, walio Wateule.” Inasema, “Walio Wateule!” Sasa, mtu ye yote, chukua Neno hilo na uliangalie pambizoni, utaona maana yake. Linasema, “Walio Wateule, waliochaguliwa tangu zamani.” Unaona? “Itam danganya kila mmoja wao ambao majina yao hayakuwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo tangu kuwekwa misingi ya dunia.”

64 Wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa, majina hayo yaliwekwa kwenye kile Kitabu. Yeye anasimama katika Mahali Patakatifu usiku wa leo, Utukufuni, kama Mwombezi, akiombea kila mmoja wa watu hao ambao majina yao yako kwenye Kitabu hicho. Na hakuna mtu anayejua jina hilo ila Yeye. Yeye ndiye



aliyeshika kile Kitabu mkononi Mwake, Naye anajua. Wakati huyo wa mwisho atakapoingia, basi siku Zake za kuombea zimekwisha. Yeye anakuja basi kudai kile Yeye alichoombea. Yeye anafanya kazi ya Mkombozi wa Jamaa wa karibu sasa; na sasa anakuja kuwapokea Walio Wake. Loo! jamani!

<sup>65</sup> Hilo linapaswa kumfanya kila Mkristo ku—kujichunguza, na kuinua mikono yake mbele za Mungu, na kusema, “Nisafishe, Ee Bwana! Yachunguze maisha yangu, na—na nijalie—nijalie kuona mahali ubaya wangu ulipo. Nijalie niundolee mbali, upesi sana.” “Kwa maana mwenye haki akiokoka kwa shida, yule asiyemcha Mungu na mwenye dhambi ataonekana wapi?” Ni wakati wa kujichunguza.

<sup>66</sup> Na kama ungetaka kuliweka, na unataka kuninii...na kutoa Neno hili.(Sasa, sitaki kuninii, kuniuliza swali juu ya jambo hili, maana linanipeleka moja kwa moja kwa lingine; ninamaanisha, katika kuandika maswali yenu. Nafikiri maswali tayari yameletwa, hata hivyo.) Huu ni wakati wa hukumu ya kuchunguza. Hiyo ni kweli. Sasa, tutapata jambo hilo kwenye—kwenye zile Baragumu tutakapofikia jambo hilo, pindi Bwana atakapotujalia, ama vile Vitasa, na tutaona kwenye hiyo hukumu ya kuchunguza, wakati kabla tu ya zile Ole kutolewa. Na—nasi tunaona ya kwamba jambo hilo ni kweli. Na wale Malaika watatu walioingia duniani, wakipaza sauti, wajua, “Ole! Ole! Ole kwa wale wakaa juu ya nchi!”

Nasi tunaishi katika wakati wa kutisha sana, wakati ambao...

<sup>67</sup> Unaona, mambo haya tuliyo ndani yake sasa, ambayo tunasoma sasa hivi, ni baada ya Kanisa kuondoka, unaona, mambo haya katika kile kipindi cha ile Dhiki. Nami nafikiri inapaswa kuwa kweli yametuliwa kweli katika kila moyo wa mwamini, ya kwamba Kanisa hili halipitii kamwe kwenye kipindi cha ile Dhiki. Huwezi kuliweka, po pote, Kanisa katika ile Dhiki. Mimi... unaliweka kanisa humo, lakini si Bibi-arusi. Unaona, Bibi-arusi ameondoka.

<sup>68</sup> Maana, unaona, Yeye, Yeye hana dhambi hata moja, hakuna hata jambo moja dhidi Yake. Neema ya Mungu imemfunika Yeye. Na kile kitakasaji kimeondolea mbali kila dhambi, hata hakuna kumbukumbu lake; hakuna kitu ila usafi, ukamilifu, katika Uwepo wa Mungu. Loo! inapaswa kumfanya Bibi-arusi kupiga magoti na kumlilia Mungu!

<sup>69</sup> Ninafikiria juu ya hadithi moja; kama sichukui wakati wenu mwingi sana sasa, katika utangulizi huu. Mimi... Ni—ninafanya jambo hili kwa kusudi fulani, kuhisi, mpaka nitakapomhisi Roho vizuri, kuanza.

<sup>70</sup> Hili ni—ni jambo takatifu. Unaona? Ni, unaona, ni nani anayejua mambo hayo pale? Hakuna mtu ila Mungu. Nayoy hayapaswi kufunuliwa, na imethibitishwa katika Biblia ya

kwamba hayangefunuliwa, mpaka ifikie siku hii. Hilo ni kweli kabisa. Unanona? Wao walikuwa—waliikisia; lakini sasa tunapaswa kuipata sawasawa kabisa, ile Kweli, Kweli iliyothibitishwa. Unaona? Angalia.

<sup>71</sup> Sasa, kulikuwako na m—msichana mdogo huko magharibi, ambaye jinsi alikuwa—alikuwa amependana na nanii... mwanamume fulani alikuwa amempenda. Kama mnunuzi wa ng'ombe, alienda sehemu hizo kwa niaba ya Kampuni ya Armour. Nao—nao walikuwa na ninii—ninii kubwa...

<sup>72</sup> Bosi alikuja siku moja, mwana wa huyo bosu kutoka Chicago, na, bila shaka, wao walivalia katika mtindo wa kawaida, wa mpakani mwa magharibi. Hao—hao wasichana kule, walivalia vizuri; kila mmoja wao alikuwa ampate kijana huyu, hakika, unajua, maana huyo alikuwa ni mvulana wa tajiri. Kwa hiyo, wao wakavalia mtindo wa mpakani mwa magharibi.

<sup>73</sup> Na—nao wanafanya hivyo huko magharibi. Karibuni wamepitia kwenye moja ya vituko hivyo. Na Ndugu Maguire, nafikiri yeye yuko hapa sasa, walimshika katikati ya mji bila nguo za kimagharibi, nao wakamtupa ko—korokoroni. Kisha wakampeleka kwenye mahakama ya mgambo, na wakamtoza faini, na halafu wakamlazimisha aende akanunue nguo za kimagharibi. Nami niliwaona wengine wao wakitembea na bunduki zenye urefu wa kiasi *hicho*, walizopakata. Wao wanaishi tu maisha ya wenyaji wa kule. Wanajaribu kuishi maisha ya siku zilizopita, zilizopita. Unaona?

<sup>74</sup> Na halafu, huko Kentucky, mnajaribu kuishi katika siku zilizopita za huku mashariki, bado mngali kule nyuma katika zama za Bonde la Renfro na kadhalika. Mnapenda kurudi nyuma kwenye siku za kale. Kuna kitu fulani kinachosababisha jambo hilo.

<sup>75</sup> Lakini wakati inapokuja kwenye kurudi, kurudi kwenye Injili ya asili, hamtaki kufanya jambo hilo. Mnataka jambo fulani la kisasa, mnaona. Inaonyesha ya kwamba, mnaona, ninyi—ninyi... kuna ninii...

<sup>76</sup> Na ni kitu gani kinachomfanya m—mtu kukosea? Ni kitu gani kinachomfanya anywe pombe na kufanya yasiyofaa, ama mwanamke kukosea? Ni kwa sababu anajaribu ku... Kuna kitu fulani ndani ya mwanamke, kinachoona kiu. Kuna kitu fulani ndani ya mwanamume, kinachoona kiu. Nao wanajaribu kutuliza hicho kiu kitakatifu kwa mambo ya ulimwengu. Ambapo, Mungu anapaswa kuwa ndiye hilo tulizo. Yeye alikuumba namna hiyo, kuona kiu. Hiyo ndiyo sababu wewe unaonea kitu fulani kiu. Mungu alikuumba namna hiyo, ili kwamba umgeuzie Yeye hicho kiu kitakatifu. Unaona? Lakini unapojaribu kutuliza hicho kiu... Mtu ye yote anathubutuje kufanya jambo hilo! Huna haki ya kufanya hivyo, kujaribu kukituliza hicho kiu kitakatifu unachoonea kiu kitu fulani, na,

halafu, nawe unakielekeza ulimwenguni, unajaribu kukituliza kwa ulimwengu. Huwezi kufanya hivyo. Kuna kitu kimoja tu kitakachojaza hicho, na hicho ni Mungu. Naye alikufanya namna hiyo.

<sup>77</sup> Kwa hiyo, huyu—wasichana hawa wadogo wakavalia m—mtindo wa kawaida wa kimagharibi kwa ajili ya mvulana huyu wakati a—alipotokea. Na kila mmoja wao alikuwa na hakika alikuwa atampata mvulana huyu.

<sup>78</sup> Palikuwapo na maskini binamu wao pale kwenye ranchi, naye alikuwa yatima, na kwa hiyo yeye alifanya tu ka—kazi zao zote. Maana, ilibidi kupaka rangi makucha yao, unajua, na hawakuweza kuosha vyombo kwa mikono na kadhalika. Naye alifanya kazi zote zilizo ngumu sana.

<sup>79</sup> Na halafu basi, hatimaye, huyo mvulana alipokuja, walienda wakamlaki katika mtindo wa kale wa kimagharibi, na gari la farasi. Nao wakaingia, wakifyatua risasi zao na kupiga makelele, unajua, na kujifanya hiki na kile. Na usiku huo walikuwa na dansi kubwa mno kule, da—dansi la mtindo wa kale, na majirani wote wanaranchi, walio karibu, na wakija na kucheza madansi kwao, na kadhalika. Na, muda si muda unajua, mbona, jambo hili liliendelea, kulikuwa na yubile kwa siku mbili au tatu.

<sup>80</sup> Halafu, usiku mmoja, mvulana huyu akatoka nje, mpaka . . . ya mahali hapo, apate kupumzika tu kidogo kutokana na hilo dansi, na akawaacha wasichana hawa. Basi ikatokea kwamba aliangalia, alipokuwa akitelemka kwenye zizi la ng'ombe. Palitokea msichana mdogo, aliyevalia kimaskini. Naye alikuwa na sufuria iliyojaa maji, aliosha vyombo. Naye akawazia, “Sikuwa nimeishamwona msichana yule hata kidogo. Sijui ametokea wapi?” Kwa hiyo akaamua kuzunguka karibu na kile—kile kibanda, na kushuka aende kule kisha arudi, karibu na lile zizi, akakutane naye.

<sup>81</sup> Huyo msichanna hakuwa na viatu. Akasimama. Akainamisha kichwa chake. Aliona huyo alikuwa ni nani, naye alikuwa na soni sana. Alimjua mtu huyu mkuu. Na msichana huyu alikuwa tu ni binamu wa hawa wasichana wengine. Baba yao alikuwa mnyapara kwenye kampuni hii kubwa ya Armour, kwa hiyo wao waliendelea . . . Aliendelea kuangalia chini. Aliona haya kwa ajili ya kutokuwa na viatu.

<sup>82</sup> Yule mvulana akasema, “Jina lako ni nani?” Yule msichana akamwambia. Akasema, “Mbona wewe huko kule kwenye ninii . . . kule waliko hao wengine?” Naye msichana kwa namna fulani akatoa udhuru.

<sup>83</sup> Na kwa hiyo, usiku wa pili, yeye alimtafuta tena. Hatimaye . . . Yule mvulana alikuwa ameketi huko nje. Na wote wakaendelea kupiga makelele, kila kitu. Yule—yule mvulana aliketi kwenye ua wa zizi la ng'ombe na kumngojea aje, kumwaga maji machafu. Naye akamngojea. Ndipo

akamwambia, akasema, “Je! unajua kusudi langu hasa la kuwa hapa?”

Yule msichana akasema, “La, bwana, sijui.”

<sup>84</sup> Kasema, “Kusudi langu la kuwa hapa ni kutafuta mke.” Akasema, “Ninaona tabia ndani yako ambayo wale hawana.” Nilikuwa nikifikiria juu ya Kanisa, unaona. Kasema, “Je! utakubali nikuoe?”

Akasema, “Ati mimi? Ati mimi? Si—siwezi kufikiria jambo kama hilo, mimi.”

<sup>85</sup> Unaona, huyo ni mwana wa tajiri mwenye mali. Yeye alikuwa ndiye tajiri wa makampuni yote na ranchi kote nchini, na kila kitu, unaona. Kasema, kasema, “Ndio.” Kasema, “Si—sikuweza kumpata mmoja huko Chicago. Ni—ninataka mke halisi. Ninataka mke mwenye tabia njema. Na kile kitu ninachotafuta ninakipata ndani yako.” Kasema, “Je! utakubali nikuoe?”

Akasema, “Vema . . .” Lilimshtusha sana msichana. Ndipo akamjibu, “Haya.”

<sup>86</sup> Na mvulana akasema, “Vema . . .” Akamwambia atarudi. Kasema, “Sasa, wewe jitayarishe, na mwaka mmoja tangu sasa nitarudi. Vema . . . Nami nitakuchukua, nami nitakuondoa mahali hapa. Haitakubidi kufanya kazi namna hii tena. Nitakuchukua. Nami nitaenda huko Chicago, na nitakujengea makazi mfano wake hujapata kuuona.

<sup>87</sup> Yule msichana akasema, “Sina ninii, sijawahi kuwa na makazi ka—kamwe. Mimi ni yatima,” akasema.

<sup>88</sup> Akasema, “Nitakujengea makazi, makazi, halisi.” Kasema, “Nitarudi.”

<sup>89</sup> Akawasiliana naye, katika wakati huo, mwaka huo. Yeye alifanya kazi kwa bidii sana alivyoweza, kuokoa fedha za kutosha katika mshahara wake wa dola moja kwa siku, ama wote aliopewa na halmashauri yake, apate kununua nguo yake ya arusi. Mfano mkamilifu wa Kanisa! Unaona? Unaona? Yeye alitayarisha mavazi yake.

<sup>90</sup> Na, unajua, wakati alipoonyesha vazi hili la arusi, binamu za—zake wakasema, “Loo!, wewe mtoto maskini mpumbavu. Unafikiri kwamba mtu kama huyo angekuwa na uhusiano wo wote na wewe?”

<sup>91</sup> Akasema, “Lakini yeye aliniahidi.” Amina. Kasema, “Yeye ameahidi.” Kasema, “Ninaamini neno lake.”

<sup>92</sup> “Loo! yeye alikuwa anakuchezea tu.” Kasema, “Kama yeye angechukua mtu ye yote, angalimchukua mmoja wao.”

<sup>93</sup> “Ndio,” kasema, “lakini yeye aliniahidi. Ninatazamia jambo hilo.” Amina. Nami, pia.

94 Kwa hiyo, siku zikazidi kupita. Hatimaye ile siku ikafika, ile saa aliyopaswa kuwa kule, kwa hiyo yule msichana akavaa lile vazi lake. Na yule msichana hata hakuwa amepata barua kutoka kwake. Lakini alijua ya kwamba angekuja, kwa hiyo akavaa mavazi yake ya arusi, akaweka vitu tayari.

95 Vema, ndipo kweli wao walicheka hapa. Maana, yule tajiri alikuwa amemtuma m—myapara, ama—ama kwa . . . Hakuna ye yote wa hao wasichana aliyekuwa amesikia lo lote juu ya jambo hilo, kwa hiyo jambo lote lilikuwa ni jambo la siri tu kwao. Hilo ni la kisiri, pia. Hakika ni la kisiri.

96 Lakini msichana huyu, mbele ya yote, juu ya msingi wa neno lake ya kwamba atarudi aje amchukue.

97 kwa hiyo, wao wakaanza kucheka. Wakakumbatiana na kuanza kumzunguka wakicheza-cheza. Wakasema “Ha!” Wakicheka, unajua, namna hiyo, wakasema, “Maskini mtoto mdogo mpumbavu!”

98 Yeye alisimama tu pale, bila kufadhaika hata kidogo. Alikuwa ameshika maua yake. Na vazi lake la arusi tayari kabisa; alikuwa amefanya kazi kwa bidiii sana, unajua. “Bibi-arusi Wake amejifanya tayari.” Unaona? Yeye alishika tu maua yake, akingojea.

99 Wao wakasema, “Sasa, nilikwambia umekosea. Unaona, yeye haji.”

Akasema, “Nina dakika nyingine tano.” Kasema, “Atawasili.”

Loo! walicheka tu!

100 Na mnamo wakati ile saa ya zamani ilipofikia dakika tano kasoro, wakasikia farasi wakienda shoti, mchanga ukivingirishwa chini ya gurudumu. Lile gari la kale la farasi likasimama.

101 Akaruka kutoka katikati yao, na huyoo akatoka mlangoni. Na yule mvulana akaruka kutoka kwenye lile gari, naye msichana akaanguka mikononi mwake. Mvulana akasema, “Yote yamekwisha sasa, mpenzi.” Akawaacha binamu zake wa kale wa kimadhehebu wameketi pale, wanaangalia. A—akaenda Chicago, nyumbani kwake.

102 Ninajua habari za ahadi nyingine kama hiyo, pia, bado. “Nimeenda kuwaandalia mahali; nitakuja kuwapokea.” Huenda wao wanasema sisi ni wenda wazimu. Lakini, ndugu, kwangu mimi, sasa hivi, na Mihuri hii ikivunjika namna hii, chini ya kitu hiki cha kimbinguni, karibu naweza kusikia sauti, ile saa ya wakati inapopiga kuelekea Umilele kule. Karibu naweza kumwona yule Malaika amesimama pale akisema, kwenye ule mwisho wa Ujumbe wa yule Malaika wa saba, “Hapatakuwa na wakati baada ya haya.” Yule Bibi-arusi mdogo, mwaminifu, ataruka kwenda kwenye mikono ya Yesu moja ya siku hizi,

akapelekwe katika Nyumba ya Baba. Hebu na tuyawazie mambo haya tunapoendelea mbele sasa.

<sup>103</sup> Angalia huduma ya simba, lile Neno; yule ndama, kazi na kujitoa sadaka; ule ujanja, wa wale watengenezaji; na wa—wakati wa tai, ukiingia, ambao utayafunua na kuyakusanya mambo haya na kuwaonyesha.

<sup>104</sup> Sasa tunaona, katika ibada ya jana usiku, pia, ile siri kuu iliyofunguliwa na Muhuri huu, jambo ambalo lilikuwa ni kinyume kabisa na ufahamu wangu wa hapo awali. Nikidhanja tu ya kwamba ilikuwa ni kweli, daima nilifikiria hizo roho chini ya madhabahu kuwa ni wale Wakristo wafia imani wa mwanzoni. Lakini tuliona, jana usiku, wakati Bwana Mungu alipotuvunja Muhuri ule, haiwezekani kabisa. Haikuwa ni wao. Wao walikuwa wamekwenda Utukufuni, moja kwa moja upande ule mwingine, na ilikuwa ndio hao hapo. Tunaona ya kwamba wao walikuwa ni Wayahudi ambao wangetokea kwa wakati huo, ambapo ninii . . .

<sup>105</sup> Kutoka kule kuitwa sasa, kwa wale mia na arobaini na nne elfu, tutakaowafikia usiku huu na kesho. Na—na kati ya Muhuri wa Sita na wa Saba, wale mia na arobaini na nne elfu wanaitwa.

<sup>106</sup> Na ndipo tunaona, ya kwamba wao walikuwa ni wafia imani ambao walikuwa wameuawa, na hata hivyo hawakuwa wameninii . . . Walikuwa wamevaa nguo ndefu nyeupe, bali majina yao yalikuwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Nao walipewa nguo ndefu nyeupe, kila mmoja wao. Nasi tulichukua jambo hilo. Na si kitu cho chote duniani, siamini, lakini ni lile kundi la—la Wayahudi waliopitia kwenye wakati fulani uliotangulia wakati wa dhiki. Wakati, kile kipindi cha wakati wa vita hivi vya mwisho, wao walikuwa . . . wao wameninii . . . Hawana budi kuchukiwa na kila mtu. Na Eichman aliua mamilioni wao huko Ujerumani. Mmesikia hayo mashtaka hivi majuzi. Mamilioni ya watu wasio na hatia waliuawa, Wayahudi, kwa sababu tu ati wao walikuwa ni Wayahudi; hakuna sababu nyingine.

<sup>107</sup> Biblia ilisema hapa, ya kwamba, “Wao waliuawa kwa ajili ya ushuhuda wao wa Mungu, kwa ajili ya Ne—Neno la Mungu, na ushuhuda waliokuwa nao.” Sasa tunaona ya kwamba Bibi—arusi alikuwa ni Neno la Mungu na ushuhuda wa Yesu Kristo. Hawa hawakuwa na ushuhuda wa Yesu Kristo.

<sup>108</sup> Nasi tunaona ya kwamba Biblia inasema, ya kwamba, “Israeli wote, Israeli waliochaguliwa tangu zamani, wataokolewa,” Warumi 11. Sasa tunajua jambo hilo. Na huko tulizona zile roho.

<sup>109</sup> Sasa angalia jinsi ilivyo karibu. Kwa nini jambo hili lisitokee hapo nyuma? Kwa sababu halikuwa limetokea hapo nyuma. Sasa unaweza kuliona, unaona. Unaona, Roho Mtakatifu aliye mkuu, akiona mambo hayo yakipitia kwenye—kwenye majira na

nyakati. Na sasa yanafunuliwa, halafu unaangalia kule na kuona hilo ni Kweli. Hapo ndipo lilipofikia.

<sup>110</sup> Sasa, ilikuwa—ilikuwa ni wale wafia imani katika ile dhiki, ama siku zilizotangulia ile dhiki, ya Eichman. Sasa, wao wanaonyesha tu mfano wa wale wafia imani mia na arobaini na nne elfu, ambao tunawaendea, kati ya Muhuri wa Sita na wa Saba. Unaona?

<sup>111</sup> Na ule Muhuri wa saba ni jambo moja tu, basi, nalo ni, “Kulikuwa kimya Mbinguni kwa muda wa nusu saa.” Na sasa ni Mungu tu anayeweza kufunua jambo hilo. Hata haujaonyesha kwa mfano, mahali po pote. Hiyo ni kesho usiku. Niombeeni. Mnaona?

<sup>112</sup> Sasa, tunaona sasa, tunapoingilia ule Muhuri wa Sita. Sasa naomba Baba wa Mbinguni atusaidie tunapotulia kwenye Muhuri huu wa Sita. Sasa aya hii ya 12 ya sura ya 6.

*Nami nikaona, alipo- . . . alipofungua muhuri ya sita, na, tazama, palikuwa na tetemeko kuu la nchi; na jua likawa jeusi kama gunia la singa, mwezi wote ukawa kama damu,*

*Na nyota za mbinguni zikaanguka juu ya . . . nchi kama vile mtini upukutishavyo mapooza yake, utikiswapo na upepo mwingi.*

*Mbingu zikaondolewa kama ukurasa uliokunjwa, na kila mlima na kisiwa kikahamishwa kutoka mahali pake.*

*Na wafalme wa dunia, na wakuu, na majemadari wakuu, na matajiri, na wenye nguvu, na kila mtum- . . . na muungwana, wakajificha katika mapango na chini ya miamba ya milima,*

<sup>113</sup> Unaona hapo? Waangalie, “watu wenye nguvu,” unaona. Walikuwa wamefanya nini? “Walikuwa wamepokea mvinyo ya hasira ya uzinzi wa yule kahaba.” Unaona? Hilo ndilo kundi lile lile lililokunywa mvinyo yake. Unaona?

*Wakiambia milima na miamba, Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso Wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo.*

*Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yake, imekuja; naye ni nani awezaye kusimama?*

<sup>114</sup> Ni utangulizi wa namna gani kuninii . . . Unaona, wale wananii wa mpanda farasi sasa, wale wanyama wa mpanda farasi, na wale Wenye Uhai wanaojibu, wamekoma. Halafu, tulichukua, tunawaona wale wafia imani chini ya kile Kiti cha Enzi. Sasa jambo hili, kutoka wakati ule, hawa wafia imani ni Wayahudi wa kweli hasa wa waliokufa katika imani ya Kikristo . . . ama ka—katika imani ya dini, kwa sababu wao hawakuweza kuwa Wakristo.

115 Kumbukeni, Mungu aliyapofusha macho yao. Nao watakuwa vipofu kwa muda mrefu, mpaka Kanisa la Mataifa litakapoondolewa. Maana Mungu hashughuliki na hao watu wawili wakati ule ule, kwa maana ni kinyume sana na Neno Lake.

116 Kumbukeni, Yeye hushughulika na Israeli kama taifa, daima. Ni taifa la Israeli.

117 Mataifa, kama watu binafsi, “watu waliotolewa kutoka kwa Mataifa.” Na ilibidi kuwa hivyo, hao Mataifa, ilibidi kufanya . . . kufanyizwa kutokana na watu wote wa ulimwenguni, kwa hiyo mara kwa mara kuna Myahudi anayeingia humo. Unaona? Kama tu vile—vile Mwarabu, Mwairishi, na Mhindi, na wengineo, ni watu wote wa ulimwenguni, wanaofanyiza shada hili la Bibiarusi. Mnaona?

118 Lakini, sasa, wakati inapofikia basi kuwashughulikia Israeli, katika sehemu hii ya mwisho ya lile juma la sabini, Yeye anawashughulikia kama taifa, Mataifa wamekwisha. Sasa karibuni imewadia, na labda kumbakia u—usiku huu huu, ambapo Mungu atawaacha Mataifa, kabisa. Kweli kabisa! Yeye alisema hivyo. “Watakanyaga kuta za Yerusalemu hata majira ya Mataifa yatakapotimia, majira yamekwisha.” Naam, bwana!

119 Na halafu, “Yeye aliye mchafu na abaki mchafu; yeye aliye mwenye haki na aendelee kutakaswa.” Unaona?

120 Hakuna Damu tena kwenye kiti cha ninii—cha ninii—cha ma- . . . mahali patakatifu, hata kidogo. Hakuna Damu tena madhabahuni. Dhabihu imeondolewa tayari, na hakuna kitu ila moshi na umeme na hukumu ndani hapo. Na hicho ndicho kabisa kilichomwagwa hapa nje usiku wa leo. Unaona, Mwana-Kondoo tayari ameondoka kwenye . . . Kazi yake ya upatanisho. Kazi ya upatanisho imekwisha, kutoka kwenye kile Kiti cha Enzi. Na ile Dhabihu, kama tulivyomwonyesha kwa mfano kikamilifu, yule Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu, yule Mwana-Kondoo aliyejaa damu ambaye alitokea. Mwana-Kondoo aliyekuwa amechinjwa, Yeye aliyejaa damu, alikuwa ameuawa, akajeruhiwa, alikuja na kukitwaa kile Kitabu kutoka katika mkono Wake. Hiyo ni kusema, siku zimekwisha. Sasa Yeye anakuja kudai kile alichokomboa. Amina! Hilo linapitisha kitu fulani ndani yangu!

121 Tunaona sasa, Yohana alisema, “Nikaona alipoufungua ule Muhuri wa Sita, palikuwa na tetemeko kuu la nchi,” ndipo maumbile yote yakakatizwa. Unaona?

122 Mungu amekuwa akifanya mambo makuu, kama kuwaponya wagonjwa, na kuyafungua macho ya vipofu, na kutenda kazi kuu.

123 Lakini tunaona, hapa, ya kwamba maumbile yalivurugika, naam, maumbile yote. Angalia yaliyotukia, “Te—tetemeko la nchi; jua likawa jeusi, na mwezi haungeangaza kutoa nuru yake; nazo nyota zikapukutika na kuanguka.” Na, mbona, kila kitu



kilitendeka, unaona, moja kwa moja kwenye ule wakati wa kufunguliwa kwa Muhuri huu wa Sita. Hapo ndipo linapotukia, pale pale mara baada ya kutangazwa kwa hao wafia imani, unaona. Wale wafia imani walikuwa wamekwisha.

<sup>124</sup> Sasa mnaona tuko karibu sana kuingia kwenye ile saa sasa. Tungeweza kuwa, wakati wo wote, unaona, kwa sababu Kanisa liko karibu tu tayari kuondoka. Lakini kumbukeni, wakati mambo haya yatakapotendeka, Bibi-arusi hatakuwa hapa. Kumbukeni tu, Bibi-arusi ameondoka, haimbidi Yeye kupitia katika yo yote ya mambo hayo. Huu ni wakati wa Dhiki, wa kusafishwa kwa—kwa kanisa; umewekwa juu yake, ili lipitie huo, si Bibi-arusi. Yeye anamwondoa mpenzi Wake. Ndiyo, bwana! Yeye, tayari Yeye amemkomboa. Unaona, ni kama ninii. . . Hilo ni chaguo Lake Mwenyewe, uchaguzi Wake Mwenyewe kama vile mtu ye yote anavyomchagua bibi-arusi wake. Mnaona? Sasa, tetemeko la nchi. . .

<sup>125</sup> Hebu na tulinganisha Maandiko sasa. Na—nataka. . . Mna penseli na kalamu? Nawatakeni mnifanyie jambo fulani. Mkitaka kuandika, andikeni jambo hili, maana, labda mwe mtachukua kanda. Sasa sisi. . . Nawatakeni msome pamoja nami, kama mnavyofanya.

<sup>126</sup> Linganisheni Maandiko ya tukio hili kuu, ili tuone siri hii kubwa, ama fumbo, lililokuwa kwenye Muhuri wa Sita wa Kitabu cha Ukombozi. Sasa kumbukeni, hizi ni siri zilizofichwa. Na ile Mihuri sita, yote kwa pamoja, ni Kitabu kimoja kikubwa, magombo sita tu yameviringishwa pamoja, nayo yanakifungua Kitabu chote cha Ukombozi. Hivyo ndivyo dunia nzima ilivyokombolewa.

<sup>127</sup> Hiyo ndiyo sababu Yohana alilia, kwa sababu, kama hakuna mtu angeweza kukipata Kitabu hicho, maumbile yote, kila kitu kilikuwa kimepotea. Hayo yangerudi tu kwa urahisi kwenye—kwenye atomi na molekuli, na kadhalika, na mialimwengu, na hata isiwe ni uumbaji mtu, cho chote kile. Maana, Adamu alipoteza haki zake za kile Kitabu. Yeye aliipoteza wakati alipomsikiliza mkewe, na yeye alisikiliza hoja za Shetani, badala ya Neno la Mungu. Unaona? Kilipotezwa.

<sup>128</sup> Halafu basi, hakingeweza kurudi kwenye mikono michafu ya Shetani, ambaye alimjaribu mwanamke akamwondoa njiani, kwa hiyo basi kilimrudia mwenyewe wa asili, kama vile hati-miliki yo yote ingefanya, unaona. Inamrudia mwenyewe wa asili moja kwa moja, na huyo alikuwa ni Mungu, Muumba, Ambaye aliitengeza. Naye ameishika.

<sup>129</sup> Na kuna gharama, na hiyo ni ukombozi. Kuna gharama fulani ya ukombozi, na hakukuwa na mtu angaliweza kufanya jambo hilo. Kwa hiyo, Yeye akasema, akaweka sheria Zake, sheria Zake Mwenyewe za Mkombozi wa Jamaa wa karibu. Ndipo, wao hawakuweza kumpata mtu ye yote. Kila mtu

alizaliwa kwa kujuana kimwili; akazaliwa kwa tamaa ya kujuana kimwili; alikuwa katika ile dhambi ya asili, Shetani na Hawa, kwa hiyo hangeweza kufanya jambo hilo. Hakuna kitu ndani yake. Hakuna papa mtakatifu, kasisi, Daktari wa Theolojia, ye yote yule awaye, hangestahili. Wala hangeweza kuwa ni Malaika, kwa maana ilipaswa awe ni Jamaa wa Karibu. Ilimbidi awe mwanadamu.

<sup>130</sup> Ndipo Mungu Mwenyewe akawa Jamaa wa Karibu, kwa kuchukua mwili wa kibinadamu, kwa kuzaliwa kibikira. Ndipo akaimwaga Damu Yake. Ile haikuwa ni damu ya Myahudi. Haikuwa ni damu ya Mmataifa. Ilikuwa ni Damu ya Mungu. Unaona? Biblia ilisema, “Tumeokolewa kwa Damu ya Mungu.”

<sup>131</sup> Mtoto huchukua damu ya babaye. Tunajua jambo hilo. Cho chote katika jinsia ya mwanamume hutoa hemoglobini. Kwa hiyo tunaona, kama vile kuku akitaga yai; anaweza kutaga yai, lakini kama jogoo, ama mwenziwe, hajashiriki naye, halitaangukiwa. Halina uhai. Mwanamke ni chombo tu cha kuatamia kinacholibeba yai. Lakini yai linatoka... Lakini ile chembechembe hai hutokana na mwanamume.

<sup>132</sup> Na, katika jambo hili, mwanamume alikuwa ni Mungu Mwenyewe. Hivyo ndivyo ninavyosema, jinsi juu ni chini, na—na kubwa ni dogo. Mungu alikuwa mkubwa sana hata akawa, hata akajitunga Mwenyewe katika kitu kidogo namna hiyo, akajifanya chembechembe ndogo sana hai ndani ya tumbo la uzazi la bikira. Na hapo Yeye akafanya seli na Damu. Naye akazaliwa, na akalelewa duniani. Na kutokana na mwanzo wa namna hiyo, usioghoshiwa, bila tamaa ya kujuana kimwili kwa jambo hilo, hata kidogo.

<sup>133</sup> Halafu akatoa hiyo Damu, kwa maana Yeye alifanyika jamaa yetu. Naye alikuwa Mkombozi aliye wa Jamaa wa Karibu. Naye akanwaga hiyo Damu, kwa mapenzi Yake Mwenyewe. Haikumlazimu kufanya hivyo. Aliitoa kwa mapenzi Yake Mwenyewe, apate kukomboa.

<sup>134</sup> Halafu anaenda kwenye madhabahu ya Mungu, na kungojea pale, wakati Mungu amekishika Kitabu cha Ukombozi mkononi Mwake. Na yule Mwana-Kondoo aliyejaa damu anasimama kwenye ile madhabahu ya dhabihu. Huyu hapo Mwana-Kondoo, kufanya ukombozi, akituombea.

<sup>135</sup> Halafu, mtu ye yote anaweza kuthubutu kusema ya kwamba Mariamu, ama Yusufu, ama mwanadamu mwingine ye yote yule, angeweza kuwa—kuwa mwombezi! Huwezi kuombea isipokuwa kuwe kuna Damu pale. Naam, bwana. “Kuna Mpatanishi mmoja kati ya Mungu na mwanadamu, na huyo ni Kristo Yesu.” Hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo. Huyu hapo amesimama, na mpaka yule mtu wa mwisho atakapokombolewa; na ndipo Yeye anakuja na kudai wale aliwakomboa. Loo! Yeye ni Baba mkuu wa—wa jinsi gani!

136 Sasa kumbukeni, sasa, daima nimefundisha, ya kwamba, “Katika vinywa vya mashahidi wawili ama watatu, kila Neno na lithibitishwe.” Na, Maandiko, kama tu vile huwezi kuchukua Andiko moja na kuthibitisha jambo lo lote isipokuwa kuna kitu kingine cha kuambatana nalo. Unaona?

137 Unaona, ninaweza kuchukua Andiko moja na kusema, “Yuda alienda zake akajinyonga,” nichukue lingine na niseme, “Nenda ukafanye vivyo hivyo.” Unaona? Lakini, unaona, halitaafikiana na mengine yote.

138 Nami nikafikiri, chini ya Muhuri huu wa Sita, wakati Roho Mtakatifu alipouvunja Huo pale, nami nikaona ulikuwa ni nini, ndipo nilifikiri lingekuwa ni jambo zuri kulipa darasa kitu kidogo tofauti usiku wa leo. Unaona? Maana, huenda ikawa inachosha, kunisikiliza tu mimi nikizungumza wakati wote, kwa hiyo nikafikiri ya kwamba tungefanya jambo fulani tofauti.

139 Sasa angalia. Tukio hili kuu lilitiwa muhuri chini ya Kitabu cha siri, cha ukombozi. Sasa Mwana-Kondoo anacho mkononi Mwake, ataivunja.

140 Sasa hebu na tuangalie Mathayo sura ya 24, Mwana-Kondoo Mwenyewe akinena. Basi, mtu ye yote anajua ya kwamba Kristo ndiye Mwandishi wa Kitabu kizima, kuhusu jambo hilo. Lakini huu ni usemi Wa—Wake hapa, ama mahubiri Ya—yake kwa wa—watu, vema, kwa Wayahudi.

141 Sasa nataka ushikilie kitabu chako namna *hii*, Mathayo 24 na Ufunuo 6, namna *hii*. [Ndugu Branham anashikilia Biblia yake imefunguliwa kwenye sura hizi mbili—Mh.] Na hebu na tulinganishe jambo fulani hapa kwa muda kidogo tu.

142 Sasa, angalia jambo hili sasa, nawe utaona vile tu ilivyo—vile ilivyo. Unaona, yale Mwana-Kondoo *hapa* anayoonyesha, katika mafumbo kabisa, ambayo Yeye alisema *hapa* katika Neno. Akifanya vile vile kabisa, kwa hiyo jambo hilo linakuwa ni sawa. Basi, ni—ni hilo tu basi. Hapa kuna . . . *Hapa* kuna moja, Yeye ananena habari zake, na *hapa* ndipo lilipotendeka. Unaona? Ni dhihirisho kamilifu tu.

143 Basi, sasa hebu na tuangalie kwenye sura ya 24 ya Mathayo, na Ufunuo 6, na tulinganishe sura ya 24 ya Mathayo. Sote tunajua ya kwamba hiyo ndiyo sura ambayo kila mwanachuoni, kila mtu anaendea, ku—kuzungumzia juu ya ule wakati wa Dhiki. Inatoka kwenye sura ya 24 ya Mathayo. Na sasa hebu tuninii . . . Kama hivyo ndivyo ilivyo, sasa sisi . . . Kwa maana, tunajua ya kwamba Muhuri huu wa Sita ni Muhuri wa hukumu. Ni Muhuri wa hukumu, ndivyo ulivyo hasa.

144 Sasa, unaona, tumekuwa na—na mpinga-Kristo akipanda na kwenda. Tumeliona kanisa likiiondoka; sasa limekwisha, linapaa juu. Halafu tunaona wale wafia imani, wa hao Wayahudi kule nyuma, chini ya madhabahu. Sasa huku ni kufumuka kwa ile hukumu, juu ya watu ambao . . .

<sup>145</sup> Kutoka kwenye hukumu hii ya ile Dhiki kutatokea wale Wayahudi mia na arobaini na nne elfu waliokombolewa. Nitawathibitishia ya kwamba wao ni Wayahudi, wala si Mmataifa. Hawana uhusiano wo wote na Bibi-arusi, hata kidogo. Bibi-arusi, tumeshaona Bibi-arusi ameshaondoka. Huwezi kuweka jambo hilo mahali pengine po pote; hawarudi tena mpaka sura ya 19 ya Kitabu cha matendo.

<sup>146</sup> Sasa angalia, kwa maana, ule Muhuri wa Sita ndio Muhuri wa hukumu ya Neno.

<sup>147</sup> Sasa, hapa, hebu na tuanze sasa na hebu na tusome Mathayo Mtakatifu, mlango wa 24. Sasa ningetaka tu kuwapa kitu fulani hapa nilichokisoma sasa hivi, kupata jambo hili. Sasa, Mathayo Mtakatifu, kutoka 1 mpaka 3, vema, ndipo tutakaposoma kwanza.

*Yesu akaenda zake, akatoka hekaluni; wanafunzi wake wakamwendea ili kumwonyesha jengo la hekalu.*

*Naye akajibu akawaambia, Hamyaoni haya yote? Amin, nawaambieni, halitasalia moja. . . halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa.*

*Sasa, hata (kifungu cha 3) alipokuwa ameketi katika. . . mlima. . . Mizeituni, wanafunzi wake wakamwendea kwa faragha, wakisema, Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? . . . ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?*

<sup>148</sup> Sasa hebu na tukomee hapo. Aya hizi tatu, zilitukia, kwa kweli, Jumanne alasiri, tarehe nne Aprili, mwaka wa 30 B.K. Na aya hizi mbili za kwanza zilitukia alasiri ya . . . Aprili nne, katika 30 B.K. Na aya ya tatu ilitukia Jumanne jioni siku ile ile. Unaona?

<sup>149</sup> Wao walikuja hekaluni, nao wakamwuliza Yeye mambo haya. “Vipi kuhusu jambo *hili*? Na vipi kuhusu jambo *hili*? Angalia hekalu hili kuu! Je! si ni la ajabu?”

Akasema, “Halitasalia jiwe juu ya jiwe.”

<sup>150</sup> Ndipo akapanda mlimani na akaketi chini, unaona. Ambapo hapo, anaanzia hapo; ni alasiri. Na halafu walipofanya hivyo, wao walimwuliza kule, kusema, “Tunataka kujua habari za mambo fulani.”

<sup>151</sup> Sasa angalia, haya hapa—haya hapa maswali matatu yaliyoulizwa na Wayahudi, mwanafunzi Wake. Maswali matatu yanaulizwa. Sasa angalia. “Mambo,” la kwanza, la kwanza, “mambo. . . Mambo haya yatakuwa lini, ni lini, ‘Halitasalia jiwe juu ya jiwe?’” “Ni nini dalili ya Kuja Kwako?” swali la pili. “Na ya mwisho wa dunia?” Unaona? Haya hapo maswali matatu.

<sup>152</sup> Sasa, hapo ndipo ambapo watu wengi wanapokosea. Wao wanayaweka mambo haya hapa katika wakati fulani wa baadaye, wakati, unaona, Yeye anajibu maswali matatu. Wao. . .

153 Angalia sasa jinsi ambavyo—jinsi jambo hili lilivyo zuri, kifungu cha 3, unaona, lile fungu la mwisho la maneno pale katika kifungu cha 3. “Na ni nini. . .” Kwanza, wao walimwita kwenye mlima wa Mizeituni hapa, kwa faragha. “Tuambie, mambo haya yatakuwa lini?” swali namba moja. “Ni nini dalili ya Kuja Kwako? swali namba mbili. “Na ya mwisho wa dunia?” swali namba tatu. Unaona? Kuna maswali matatu mbalimbali yaliyoulizwa. Basi, sasa nawataka mfungue na mwone jinsi Yesu hapa anavyoambia juu ya mambo haya.

154 Loo! ni zuri sana! Mimi. . .Linanifanya tu mimi. . . Ni—ni—ninapata ninii. . .Ilikuwa ni neno gani lile tulilotumia juzijuzi usiku? [Kusanyiko, “Changamko.”—Mh.] Changamko linalotokana na ufunuo! Angalia.

155 Sasa hebu na tufungue sasa kwenye Muhuri wa Kwanza wa—wa Mihuri ya Kitabu hiki, na tulinganishe Muhuri huu wa Kwanza na swali hili la kwanza.

156 Na kila swali, tulilinganishe kote kote, na tuone kama haliambatani, kama tu tulivyofanya katika huku kufunguliwa kwa hii mingine, kwenye nyakati za kanisa na kila kitu, kitu kile kile kabisa. Huo hapo ule Muhuri, umefunguliwa kikamilifu, basi. Angalia, sasa. Sasa tutasoma, kwanza, kwa ninii. . . “Ndipo Yeye akajibu akawaambia. . .” Na—na halafu Yeye—Yeye ataanza kujibu sasa, nasi tunataka kulinganisha hilo na ile Mihuri.

157 Sasa angalia. Muhuri wa kwanza ni Ufunuo 6:1 na 2. Sasa tusome 6:1 na 2.

*Kisha—kisha nikaona. . .Mwana-Kondoo hapo alipofungua moja ya zile muhuri saba, na nikasikia mmoja wa wale wenye uhai wanne akisema, kama kwa sauti ya ngurumo, Njoo uone.*

*Nikaona, na tazama, farasi mweupe, na yeye aliyempanda ana uta, akapewa taji, naye akatoka, ali akishinda tena apate kushinda.*

158 Tuliona jamaa huyu alikuwa ni nani? [Kusanyiko linasema, “mpinga-Kristo.”—Mh.] Mpinga-Kristo. Mathayo 24, sasa, 4 na 5.

*Yesu akajibu, akawaambia,—akawaambia, Angalieni, mtu asiwadanganye.*

*Kwa sababu wengi watakuja kwa jina Langu, wakisema, Mimi ni Kristo; nao watadanganya wengi.*

159 Mnaona hilo? Mpinga-Kristo. Huo hapo Muhuri wako. Unaona? Unaona? Yeye aliuzungumzia habari zake hapa; na hapa wao wanafungua Muhuri, naye alikuwa ndiye huyu hapa, kikamilifu tu.

160 Sasa Muhuri wa Pili, Mathayo 24:6, Ufunuo 6:3 na 4. Sasa angalia. Mathayo 24:6. Sasa hebu nione inavyosema.

*Nanyi mtasikia habari ya vita na matetesi ya vita; angalieni, msitishwe; maana hayo hayana budi kutukia; lakini ule mwisho bado.*

<sup>161</sup> Vema, hebu na tuchukue Muhuri wa Pili, Ufunuo 6:3 na . . . Ya pili. Angalia anavyosema sasa.

*Na alipoifungua muhuri ya pili, nikamsikia yule mwenye uhai wa pili akisema, Njoo uone.*

*Akatoka farasi mwingine, mwekundu sana, na yeye aliyempanda alipewa kuiondoa amani katika nchi, ili watu wauane, naye akapewa upanga mkubwa.*

<sup>162</sup> Kabisa, barabara kabisa! Loo! ninapenda kuyafanya Maandiko yajijibu Yenyewe. Na ninyi je? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Roho Mtakatifu aliyaandika yote, lakini Yeye anaweza kuyafunua.

<sup>163</sup> Sasa hebu na tuone Muhuri wa Tatu. Sasa, hii ni njaa. Sasa, Mathayo 24:7 na 8. Hebu tufungue 7 na 8, katika Mathayo.

*Na taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na njaa, . . . tauni, . . . matetemeko ya nchi mahali mahali.*

*Mambo hayo yote ndiyo mwanzo wa utungu.*

<sup>164</sup> Unaona, unakuja moja kwa moja sasa. Sasa, Ufunuo, katika ya 6, sasa tunaenda kufungua Muhuri wa Tatu. Unapatikana katika Ufunuo 6:5 na 6.

*Na alipoifungua muhuri ya tatu, ni—nikaona yule wa tatu mwenye uhai akisema, Njoo uone! Nikaona, na tazama, farasi mweusi, na yeye aliyempanda ana mizani mkononi mwake.*

*Nikasikia kama sauti katikati ya hao wenye uhai wanne, ikisema, Kibaba . . . nusu rupia . . . kibaba cha ngano kwa nusu rupia, na vibaba vitatu vya shayiri kwa nusu rupia, wala usiyadhuru mafuta wala . . . divai.*

<sup>165</sup> Njaa! Unaona, ni Muhuri ule ule hasa, jambo lile lile alilosema Yesu. Vema.

<sup>166</sup> Muhuri wa Nne, “tauni” na “mauti.” Angalia, Mathayo 24. Tutasoma a—aya ya 8, ya 7 na ya 8, naamini ndiyo, kwenye Muhuri huu wa Nne, nilio nao hapa. Vema.

<sup>167</sup> Sasa, nilisoma nini hapa nyuma? Je! nilisoma kitu kingine? Naam, nilikuwa nimetia hicho alama. Naam, basi. Sasa tutaenda. Sasa twende. Vema, bwana.

<sup>168</sup> Sasa hebu na tuanzia hapa kwenye cha 7, kwenye huu, Muhuri wa Nne; na katika kifungu cha 6:7 na cha 8, kwenye hicho kingine, kwenye Ufunuo.

<sup>169</sup> Sasa hebu na tuone aya ya 7 na ya 8 ya Mathayo 24. Vema, sasa.

*Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; na kutakuwa na njaa, . . . tauni, . . . matetemeko ya nchi mahali mahali.*

*Hayo yote ndiyo mwanzo wa utungu.*

170 Sasa ule Muhuri wa Nne, kama tulivyousoma hapa, ulikuwa hii. . . Muhuri wa Nne, ulianza kwenye cha 7 na cha 8, kwenye hiki kingine sasa.

*Na alipoifungua muhuri ya nne, na tazama . . . nikasikia sauti ya yule mwenye uhai akisema, Njoo uone!*

*Nikaona, na tazama, farasi wa rangi ya kijivujivu . . .*

171 Sasa ngoja. Niliandika hili vibaya. Naam. Naam. Sasa hebu kidogo, sasa, cha 7 na cha 8.

172 Sasa hebu tuone, Mathayo 24:7 na cha 8. Sasa hebu tuone. Tatalipata hilo. Huo ni wa Tatu, kufunguliwa, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mathayo 24:7 na ya 8. Samahani. Sasa, hiyo inafungua mvua . . . ama njaa, inafungua njaa. Vema.

173 Sasa, "tauni" na "mauti." Naam, bwana. Sasa tutakiendea, cha 7 na cha 8. Sasa, huo ungekuwa ni Muhuri wa Nne. Hebu na tuone mahali tunapoupata Muhuri wa Nne." Na alipoifungua Muhuri—Muhuri ya Nne. . . " Naam, ni yule mpanda farasi wa kijivujivu, "Mauti," unaona.

*Na—na nikaona, na tazama, farasi wa rangi ya kijivujivu, na yeye . . . farasi wa rangi ya kijivujivu, na yeye aliyempanda jina lake ni Mauti, na Kuzimu akafuatana naye. Nao wakapewa mamlaka juu ya ro- . . . robo ya nchi, waue kwa upanga na kwa njaa na kwa tauni na kwa hayawani wa nchi.*

174 Sasa, mnaona, hiyo ilikuwa ni "Mauti."

175 Sasa, Muhuri wa Tano, Mathayo 24:9-13. Hebu tuone kama nimelipata hili vizuri, sasa, tena. Unaona?

*Wakati huo watawasaliti ninyi mpate dhiki, nao watawaua (haya basi); nanyi mtakuwa watu wa kuchukiwa na mataifa yote kwa ajili ya jina langu. Na hapo . . .*

*Ndipo wengi watasaliti- . . . wengi watakapojikwaa, nao watasalitiana na kuchukiana.*

*Na manabii wengi wa uongo watatokea, na kudanganya wengi.*

*Na kwa sababu ya kuongezeka maasi, upendo wa wengi utapoa.*

*Lakini mwenye . . . mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayekoka.*

176 Sasa, tuko kwenye Muhuri wa Tano sasa. Na huo ulikuwa ni usiku wa jana, unaona. “Watawasaliti, watasalitiana,” na kadhalika.

177 Sasa angalia hapa kwenye ya 6, Muhuri, 6:9 mpaka 11. Sasa hebu tuendee huo, Ufunuo 6:9 hadi 11..

*Na alipoifungua muhuri ya tano, nikaona chini ya madhabahu roho zao waliochinjwa kwa ajili ya neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao.*

*Wakalia kwa sauti kuu, wakisema, Ee Mola, Mtakatifu, . . . Mwenye kweli, hata lini, . . . kutokuhukumu, wala kuipatia haki damu yetu kwa hao wakaao juu ya nchi?*

*Basi, nao wakapewa kila mmoja nguo ndefu, nyeupe, na wakaambiwa wastarehe bado muda mchache, hata itakapotimia hesabu ya wajoli wao na ndugu zao, . . . watakaouawa vile vile kama wao.*

178 Sasa, unaona, chini ya Muhuri wa Tano, tunaona—tunaona hapa mauaji ya wafia imani.

179 Na chini ya 24:9 hapa, tu- . . . mpaka 13, tunaona pia ya kwamba walikuwa ni mfia imani. “Watawasaliti, na kuwaua,” na kadhalika. Unaona, ni muhuri ule ule ukifunguliwa.

180 Sasa, katika Muhuri wa Sita, ndio ule tunaouendea sasa, Mathayo 24:29 na 30. 24, na hebu tufungue 29 na—na 30. Huyu hapa.

Sasa, sasa tutafungua, pia, Ufunuo 6:12 mpaka 17.

181 Hayo ndiyo yale hasa tuliyosoma tu sasa hivi. Sasa sikilizeni hili, sasa, yale aliyosema Yesu katika Mathayo . . . :29, 24:29 na 30.

*Lakini mara, baada ya dhiki ya siku zile, . . .*

182 Ati nini? Wakati ninii..dhiki hii, dhiki hii ndogo ambayo wamepitia hapa, unaona.

*. . . jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota zitaanguka kutoka mbinguni, na nguvu za . . . mbinguni zitatikisika;*

*Ndipo itakapoonekana ishara yake Mwana wa Adamu mbinguni; ndipo itakuwa mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi.*

183 Sasa, soma hapa katika Ufunuo sasa, ule—ule Muhuri wa Sita, ule tulio nao sasa hivi.

*Nami . . . tazama, alipoifungua muhuri ya sita, na, tazama, palikuwa na tetemeko kuu la nchi; na jua likawa jeusi kama gunia (unaona?) la singa, na mwezi wote ukawa kama damu,*



*Na nyota za mbinguni zikaanguka juu ya nchi kama vile mtini upukutishavyoa mapooza yake, utikiswapo na upepo mwingi.*

*Mbingu zikaondolewa kama ukurasa unavyokunjwa, na kila mlima na kisiwa kikahamishwa kutoka mahali pake.*

*Na wafalme wa dunia, na wakuu, na majemadari wakuu, na matajiri, na wenye nguvu, na kila mtumwa, . . . na mwungwana, wakajificha katika mapango chini ya miamba ya mlima,*

*Wakiiambia milima na miamba, Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira—hasira ya Mwana-Kondoo.*

*Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yake, imekuja; . . . ni nani awezaye kusimama?*

184 Ni sawa kabisa, tufungue upande huu mwingine, tuone vile Yesu alivyosema hapa sasa katika Mathayo 24:29. Sikilizeni. “Baada,” hiki kisa cha Eichman, na kadhalika.

*Lakini mara, baada ya dhiki ya siku zile, jua litatiwa giza, . . . mwezi hauta—hautatoa mwanga wake . . . nyota zitaanguka kutoka mbinguni, . . . nguvu za mbinguni zitatikisika;*

Sasa angalia.

*Ndipo itakapoonekana ishara yake Mwana wa Adamu Mbinguni; nao wataona, nao . . . ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi.*

*Na . . . atawatuma malaika zake na kadhalika, na pamoja na sauti ya parapanda, na . . . watawakusanya wateule wake . . . pepo nne . . . , kushindana pamoja.*

185 Unaona, ni kitu kile kile hasa, kulinganisha yale Yesu aliyosema katika Mathayo 24, na yale mfunuzi hapa aliyofungua kwenye Muhuri wa Sita, ni sawa kabisa. Na Yesu alikuwa akinena juu ya ule wakati wa Dhiki. [Ndugu Branham anagonga-gonga mimbarani mara tatu—Mh.] Unaona?

186 Kwanza, yeye aliwauliza mambo haya yatakuwa lini, wakati hekalu lingeondolewa. Alijibu hilo. Jambo lingine alilouliza, ni lini ungekuja wakati . . . Ungekuja wakati wa wafia imani. Na wakati hili lingetukia, wakati mpinga-Kristo angeinuka; na wakati mpinga-Kristo angeliondoa hekalu.

187 Danieli, jinsi tungeweza kurudi na kuchukua Danieli pale, wakati aliposema jambo hilo, huyu mtawala ambaye angekuja. Ninyi wasomaji mnajua jambo hilo. Naye atapaswa kufanya

nini? Angeondoa dhabihu ya kila siku, na yale yote yangetukia kwenye wakati huo. Kasema. . .

188 Yesu, hata Yeye, akinena juu ya jambo hilo hapa, alilitilia mkazo. Alisema, “Hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu, lile lililonenwa na nabii Danieli, limesimama katika patakatifu.” [Ndugu Branham anagongagonga mimbara mara tatu—Mh.] Ni kitu gani hicho? Ule msikiti wa Omar, ulisimama mahali pa lile hekalu wakati walipoliteketeza kwa moto. Alisema, “Walio milimani. . .Walio juu ya dari, wasishuke kuvichukua vitu vilivyomo nyumbani mwao, wala aliye shambani asirudi nyumbani. Kwa maana wakati huo kutakuwako dhiki kubwa!” Mnaona? Na mambo haya yote yangetokea, akawapeleka sasa na kulithibitisha, akawarudisha kwenye huku kufunguliwa kwa Muhuri wa Sita.

189 Sasa nataka mwone. Yesu. . .Sasa, kesho kama usiku hivi, kuhusu Huu, Yesu aliacha kuufundisha ule Muhuri wa Saba. Haupo hapa. Angalia, Yeye anaendelea moja kwa moja na mifano sasa, baada ya jambo hilo. Naye Yohana aliacha Muhuri wa Saba. Ule wa Saba, wa mwisho, ule Muhuri wa Saba, hilo litakuwa ni jambo kubwa. Hata haujaandikwa, unaona. Waliacha Muhuri wa Saba; wote wawili waliuacha. Na yule mfunuzi, wakati Mungu aliposema tu kwamba kulikuwako. . . Yohana alisema, “Kulikuwa tu na kimya Mbinguni.” Yesu hakusema neno kamwe juu Yake.

190 Angalia sasa, turudi nyuma kwenye ile aya ya 12, angalia, hakuna Mwenye Uhai. Hiyo ni aya ya 12, tukiianza Muhuri wetu, kuuona ukifunguliwa. Hakuna Mnyama, kama vile, Wenye Uhai, aliyewakilishwa hapa, hapana, kama ilivyokuwa kwenye ule Muhuri wa Tano. Kwa nini? Jambo hili lilitukia, ng’ambo ya pili ya wakati wa Injili, katika wakati wa ile Dhiki. Huu Muhuri wa Sita ni wakati wa ile Dhiki. Hilo ndilo linalotukia. Bibi-arusi ameondoka. Unaona? Hakuna Mwenye Uhai wala kitu cho chote pale kusema jambo hilo. Ni ninii tu. . .Sasa, Mungu halishughulikii Kanisa tena. Limeondoka tayari.

191 Yeye anawashughulikia Israeli, unaona. Unaona, hii ni kule ng’ambo, huu ni wakati Israeli ilipoupokea Ujumbe wa ufalme, kwa wale manabii wawili wa Ufunuo 11. Kumbukeni, Israeli ni taifa, mtumishi wa Mungu, taifa. Na wakati—wakati—wakati Israeli itakapoingizwa, itakuwa ni—ni mambo ya taifa.

192 Israeli, ule wakati wa ufalme, ni wakati ambapo Daudi. . . Mwana wa Daudi, anapoketi kwenye kiti cha enzi. Hiyo ndiyo sababu yule mwanamke alilia, “Ewe Mwana wa Daudi!” Naye Daudi ataninii. . .Mwana wa Daudi! Mungu alimwambia kwa Yeye, kwa Daudi, ya kwamba Yeye angemwinulia Mwanawe ambaye angekitwaa kiti chake cha enzi. Kingekuwa ni kiti cha enzi cha milele. Unaona? Hakingekuwa na mwisho. Sulemani alikitoa, katika mfano, hekaluni. Naye Yesu aliwaambia tu hapa,

ya kwamba, “Halitasalia jiwe juu ya moja ya hayo.” Lakini Yeye anajaribu kuwaambia hapa, kile . . . Yeye anarudi.

“Utarudi lini?”

193 “Mambo haya yatatukia kabla sijarudi.” Nayo ni ndiyo haya hapa!

Sasa tuko katika wakati wa ile Dhiki.

Kumbukeni, wakati ule ufalme utakapozishwa, juu ya nchi . . .

194 Sasa, hili linaweza likawa kidogo linashtusha. Na endapo kuna swali, basi u—ungali unaweza kuniuliza; kama ukitaka kukuliza hilo swali, baada ya hilo kuitwa, na uliulize tu; kama hukufahamu, kama hulijui bado.

195 Katika ule wakati wa Utawala wa Miaka Elfu, Israeli ndio taifa, yale makabila kumi na mawili kama taifa.

196 Lakini Bibi-arusi yuko kwenye jumba la kifalme. Yeye ni Malkia sasa. Ameolewa. Na dunia yote itakuja kwenye mji huu, Yerusalemu, na kuleta utukufu wake mle. “Nayo malango hayatafungwa, usi—usi—usiku, maana hakutakuwako na usiku wo wote.” Unaona? Malango yatafunguliwa daima. “Na wafalme wa nchi,” Ufunuo. . . 22, “wataleta heshima zao na utukufu kwenye mji huu.” Lakini Bibi-arusi yuko ndani kule pamoja na Mwana-Kondoo. Loo! jamani! Unaweza kuona jambo hilo, kule ndani! Si . . . Bibi-arusi hatakuwa nje hapa akifanya kazi kwenye mashamba ya mizabibu. La, bwana. Yeye ni Bibi-arusi. Yeye ni Malkia wa yule Mfalme. Hao wengine ndio wanaofanya kazi kule nje, lile taifa, si Bibi-arusi. Amina. Vema.

197 Angalia wajumbe hawa sasa, wajumbe hawa wa Ufunuo . . . :12, manabii hawa wawili, wao watahubiri, “Ufalme umekaribia!” Unaona? Ufalme wa Mbinguni utanzishwa. Ule wakati, ile miaka mitatu na nusu ya mwisho ya juma la sabini la Danieli, iliyoahidiwa Wayahudi, watu Wake. Kumbuka sasa, ya kwamba, kuthibitisha jambo hilo, ya kwamba hii ni sehemu ya mwisho ya juma la sabini la Danieli. Nina swali juu ya jambo hilo kwa ajili ya kesho. Unaona?

198 Sasa, majuma sabini yaliahidiwa, ambayo yalikuwa ni miaka saba. Na katikati ya majuma saba, Masihi angekatiliwa mbali, kufanywa dhabihu. Yeye angetabiri kwa muda wa miaka mitatu na nusu, na halafu ndipo angekatiliwa mbali, kwa ajili ya dhabihu ya watu. Na kungali kumekusudiwa, hiyo miaka mitatu na nusu ingali imekusudiwa Israeli. Halafu, wakati Masihi alipokatiliwa mbali, Myahudi alipofushwa hivi kwamba asingeweza kuona huyo alikuwa ndiye Masihi.

199 Na, basi, wakati Masihi alipokatiliwa mbali, basi wakati wa neema ya Injili ulimjilia Mmataifa. Nao wakaja, Na Mungu akamtoa mmoja kutoka *hapa* na *pale*, na *hapa* na *pale*, akawaondoa na kuwaweka chini ya hao wajumbe; na *hapa*

na *pale*, na *hapa* na *pale*, na kuwaweka mbali chini ya wale wajumbe.

<sup>200</sup> Ndipo akamtuma mjumbe wa kwanza, naye akahubiri, na baragumu ikalia; kama tutakavyolichukua, baada ya kitambo kidogo. Na, basi, hiyo baragumu ilikuwa ikitangaza vita. Baragumu daima humaanisha vita. Yule mjumbe, yule malaika alikuja duniani, yule mjumbe wa saa, kama vile Luther, kama ye yote wa wale wajumbe ambao tumenena habari zao. Mjumbe anafanya nini? Anawasili; na Muhuri unafunguliwa, unafunuliwa; baragumu inalia, vita vinatangazwa, na hao wanaondoka. Na ndipo huyo mjumbe anakufa. Yeye anatia muhuri kundi hili; wanaingizwa. Kisha mapigo yanawaangukia hao walioukataa. Unaona?

<sup>201</sup> Ndipo inaendelea, halafu wanaunda madhehebu, wanapata madhehebu mengine. Ndio tu tumeishapitia jambo hilo. Halafu, hawa hapa wanakuja na nguvu nyingine, unaona, nguvu nyingine, wakati mwingine wa kanisa, huduma nyingine. Ndipo, wakati anapofanya hivyo, Huyu hapa Mungu anakuja na huduma Yake, wakati mpinga-Kristo anapotokea na yake. Unaona, *mpinga* ni “kinyume.” Wanaenda sambamba.

<sup>202</sup> Nawatakeni mwone jambo fulani dogo. Yapata tu wakati ambapo—ambapo Kaini alikuja duniani, Habili alikuja duniani. Ninataka mwone, yapata tu wakati ambapo—ambapo Kristo alikuja duniani, Yuda alikuja duniani. Yapata tu wakati ambapo Kristo aliondoka duniani, Yuda aliondoka duniani. Yapata tu wakati ambapo Roho Mtakatifu alishuka, roho ya mpinga-Kristo ilishuka. Yapata tu wakati ambapo Roho Mtakatifu anajifunua hapa katika siku za mwisho, mpinga-Kristo anaonyesha rangi zake, akija kupitia katika siasa zake na kadhalika. Na yapata wakati ambapo mpinga-Kristo anajitokeza mwenyewe kikamilifu jukwaa- . . . jukwaani; Mungu anajitokeza kikamilifu jukwaani, kuvikomboa vitu vyote. Unaona, inaenda tu, moja pamoja tu. Nao, wote wawili, wako sambamba. Kaini na Habili! [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.] Kunguru na njiwa, kwenye safina! Yuda na Yesu! Na kuendelea tu mbele, unaweza kulichukua. Ninii tu.

<sup>203</sup> Hapa walikuwapo Wamoabu na Israeli; wote wawili. Moabu halikuwa taifa la kikafiri. La, bwana. Wao walitoa dhabihu ile ile Israeli waliyokuwa wakitoa. Walimwomba Mungu yule yule. Kweli kabisa. Moabu aliitwa . . . Alikuwa mmoja wa binti za Lutu ambaye alilala na baba yake, na akapata mtoto. Na mtoto huyo aliitwa Moabu. Na kutoka kwake ikatokea jamii ya Moabu, nchi ya Moabu.

Na wakati walipowaona Israeli, ndugu yao aliyekombolewa, akija.

<sup>204</sup> Wao walikuwa ni watu wa kimsingi. Walikuwa ni madhehebu makubwa. Israeli hawakuwa na madhehebu;

waliishi tu katika mahema na popote pale. Lakini Moabu alikuwa na watu mashuhuri, wafalme, na kadhalika. Na walikuwa na Balaamu kule juu, nabii wa u—uongo. Pia walikuwa na haya yote. Basi wakashuka wakaja kule kumlaani ndugu yao mdogo aliyekuwa akienda zake kwenye nchi ya ahadi, akienda kwenye ahadi yake.

<sup>205</sup> Basi akaenda na akawauliza, “Je! ninaweza kupita katika nchi yenu? Kama ng’ombe wangu wakinywa maji, nitayalipa. Kama wakila nyasi, tutazilipa.”

<sup>206</sup> Akasema, “La. Hamtafanya uamsho wa namna hiyo hapa. Hiyo ni kweli. Hamtaendeleza jambo kama hilo mahali hapa.”

<sup>207</sup> Na basi angalia yale aliyofanya. Alirudi moja kwa moja katika mfano wa Yezebeli, na akaja kupitia kwa huyo nabii wa uongo, na kuwasababisha watoto wa Mungu kukosea. Kisha akawaoza wanawake wa Kimoabu kwa—kwa Israeli, na kusababisha uzini.

<sup>208</sup> Na yeye alifanya jambo lile lile, katika wakati ule ule, safarini, wakielekea kwenye Nchi ya ahadi, tunakoelekea. Yeye alifanya nini? Yule nabii wa uongo alikuja moja kwa moja na kuwaoza, na kuingia kwenye kanisa la Kiprotestanti, na kuanzisha madhehebu, kama vile vile tu walivyofanya kule nyuma. [Ndugu Branham anagongagonga mimbara mara nne.]

<sup>209</sup> Lakini maskini Israeli wa zamani alisonga mbele, hata hivyo. Walinung’unika jangwani kwa muda mrefu, na wale mashujaa wa kale wote ilibidi wafe, lakini waliendelea moja kwa moja mpaka kwenye nchi ya ahadi. Naam. Ndiyo. Waangalie wote wakiwa na zana za vita, kabla tu hawajauvuka Yordani. Ha—ha! Napenda jambo hilo. Sasa tunafikia kwenye wakati huo sasa hivi, hapa sasa hivi. Angalia.

<sup>210</sup> Sasa tunaona, ya kwamba, ule wakati, ile miaka (nilisema) mitatu na nusu ya mwisho ya majuma sabini ya Danieli.

<sup>211</sup> Hebu nielezee jambo hilo kwa makini kidogo sasa, maana ninamwona mtu fulani hapa ambaye daima amechunguza jambo hilo, nami—nami nataka kujaribu kuwa wazi; mwalimu fulani.

<sup>212</sup> Angalia wakati yale majuma sabini yalipoingia. Wakati Danieli alipoona lile ono la wakati ujao, na mwisho wa Wayahudi, lakini alisema majuma sabini yalikuwa yamekusudiwa. Hiyo ni miaka saba; katikati yake, mbona, Masihi atakuwa yupo hapa, ama, naye angekatiliwa mbali, kwa ajili ya dhabihu. Sasa, hilo ndilo lililotukia hasa.

<sup>213</sup> Halafu, Mungu aliwashughulikia Mataifa hata wakachukua watu kwa ajili ya Jina Lake. Mara Kanisa la Mataifa linapoondolewa, Yeye alilinyakua Kanisa.

<sup>214</sup> Na wakati alipofanya hivyo, yule mwanamwali aliyelala, kanisa lenyewe. . . Bibi—arusi alipaa juu. Nalo kanisa likawekwa katika “giza la nje, ambako kuna kulia, na kuomboleza, na

kusaga meno.” Katika wakati ule ule, ile Dhiki inawaangukia watu hao.

<sup>215</sup> Na wakati ile Dhiki inaposhuka, katika wakati huo wanakuja hawa manabii wawili wa Ufunuo 11, kuwahubiria Injili. Nao wanahubiri elfu moja, mia moja. . . na siku sitini. Mnaona? Vema, hilo ni sawa kabisa, kukiwako na siku thelathini kwa mwezi kama kalenda halisi ilivyo nazo, ni miaka mitatu na nusu hasa. Hiyo ndiyo sehemu ya sabini ya Danieli, ile sehemu ya mwisho ya juma la sabini. Unaona?

Mungu hajawashughulikia Israeli hapa. La, bwana.

<sup>216</sup> Ndugu fulani aliniuliza, si muda mrefu uliopita, kasema, “Je! niende. . .” Ndu—ndugu mmoja hapa kanisani, ndugu wa thamani, mpendwa, alisema, “Na—nataka kwenda Israeli. Ninaamini kuna uamsho.”

<sup>217</sup> Mtu fulani aliniambia, “Ndugu Branham, unapaswa kwenda Israeli sasa hivi. Wao wangeona hilo.” Unaona, huwezi kufanya hivyo.

Nilisimama pale pale, nami nikawazia. . .

<sup>218</sup> Hao Wayahudi walisema, “Kama mimi. . . Vema, kama huyu ni, Yesu akiwa—akiwa ndiye Masihi,” kasema, “hebu nimwone akifanya ishara ya nabii. Tutaamini manabii wetu, maana hivyo ndivyo wanavyopaswa—wanavyopaswa kuwa.”

<sup>219</sup> “Ni mpango mzuri namna gani,” nikawazia. “Mimi naenda!” Nilipofika pale pale, karibu sana na huko, moja kwa moja. . . Nilikuwa, vema, nilikuwa Cairo. Nami nilikuwa nimeshika tikiti yangu mkononi, ya kwenda Israeli. Nami nikasema, “Mimi, nitaenda, nione kama watauliza jambo hilo, kama wanaweza kuona ishara ya nabii. Tutaona kama wao watamkubali Kristo.”

<sup>220</sup> Lewis Pethrus, wa kanisa la Stockholm, aliwatumia Biblia milioni moja.

<sup>221</sup> Na hao Wayahudi wakija pale! Mmeona ile sinema. Ninayo kwenye ukanda, papa hapa sasa, *Usiku wa Manane Kasoro Dakika Tatu*. Na hao Wayahudi wakiingia, kutoka kila mahali ulimwenguni, kila mahali, wanaanza kukusanyika kule.

<sup>222</sup> Baada ya Uingereza kwenda kule, katika wakati wa Jemadari Allenby. Katika *Kule Kumalizika Kwa Vita Vya Dunia*, katika kitabu cha pili, nafikiri ndicho. Nao wakajisalimisha, Waturuki walijisalimisha. Ndipo akairudisha kwa Israeli. Nayoyamekuwa ikikua kama taifa, na sasa hilo ni taifa kamili: fedha zake lenyewe, sarafu, bendera, jeshi, na cho chote kile. Unaona?

<sup>223</sup> Na hawa Wayahudi, wakirudi kwenye nchi ya uenyeji wao, wao walikuwa. . . Jambo la kwanza, waliposhuka kwenda Iran, na kwenye nchi ile, kuwachukua, wao waliuliza. . . Walisema yeye. . . Wanawataka wawarudishe nchini Israeli, kuwapa nchi yao; kuwarudisha kwenye nchi yao, Palestina, mahali wanapapaswa kuwa.

224 Na, kumbukeni, mradi tu Israeli wako nje ya nchi hiyo, wao wako nje ya mapenzi ya Mungu; kama vile Ibrahimu, ambaye alipewa hiyo nchi. Na wakati . . .

225 Wao walikataa kuingia kwenye hiyo ndege. Hawakuwa wameshaona kitu cha namna hiyo. Kulikuwa na maskini rabi mzee aliyetokeza pale, akasema, “Nabii wetu alituambia, ya kwamba, wakati Israel watakapoenda nyumbani, itakuwa ni kwenye ‘mbawa za tai,’” katika ndege, wakienda zao nyumbani.

226 Ndiye huyo hapo hivi sasa, akijenga. Mtini ukirudishwa! Amina! Ile nyota yenye ncha sita ya Daudi ikipepea!

227 “Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa na hofu!” Ule wakati wa Dhiki umekaribia sana!

228 Nasi tukisimama papa hapa, na ile Mihuri ikifunguliwa, Kanisa likiwa tayari kwenda Zake kuruka hewani!

229 Na ile Dhiki ikianza, ndipo Mungu anashuka na kuwatoa wale mia na arobaini na nne elfu kutoka kule. Amina! Hapo, loo! ni kamilifu! Unaona mahali ile Mihuri inapolifafanua sasa, unaona, kulifungua jambo hilo? Sasa, hii ni ile miaka mitatu na nusu ya mwisho kwa wale watu. Pia, kama ukiangalia, ndio wakati ambapo Mungu atawaita wale Wayahudi mia na arobaini na nne elfu, katika hii miaka mitatu na nusu.

230 Unaona, Yeye hajawashughulikia, hata kidogo. Hawajakuwa na nabii. Hawataamini kitu kingine ila nabii. Huwapumbazi. Kwa hiyo, wao watamsikia nabii, naam, bwana, na ni hayo tu. Hilo, Mungu aliwaambia hilo hapo mwanzo, nao wanadumu moja kwa moja nalo.

231 Yeye alisema, “Bwana Mungu wako atawaondokeshea Nabii kati yenu, kama nilivyo mimi.” Musa alisema jambo hilo. Kisha akasema, “Huyo mtamsikia. Na kila ambaye hatamsikia Nabii huyo, atakatiliwa mbali na watu.” Hiyo ni kweli.

232 Na, mnaona, macho yao ilibidi yapofushwe, la sivyo wao wangelimtambua Yeye. Badala yake, wakiwa wamepofushwa, wao walikuwa . . . Hilo lilimwacha Shetani awapate, nao wanasema, “Yeye ni mpiga ramli, Beelizebuli. Damu Yake na iwe juu yetu. Tunajua Yeye hana lo lote.” Mnaona?

233 Na maskini watu hao walipofushwa. Hiyo ndiyo sababu lile kundi la Eichman na kundi hilo lote lililouawa kule nyuma. Walikuwa na haki ya kuingia; ilimbidi Baba yao Mwenyewe kuyapofusha macho yao ili kwamba apate kutuchukua sisi.

234 Hilo ndilo jambo la huzuni sana katika Maandiko, kwa kweli. Wazia tu juu ya pale, hao Wayahudi, wakiililia Damu ya Baba yao wenyewe, Mungu wao wenyewe akining’inia pale, akitokwa na damu. Angalia, “Hapo wao wakamsulubisha Yeye,” Biblia ilisema. Hayo ndiyo maneno manne ya maneno yaliyo makuu kuliko yote. Angalia. “Hapo,” Yerusalemu, mji ulio mtakatifu sana ulimwenguni. “Wao,” watu walio

watakatifu sana ulimwenguni. “Wakamsulubisha,” kifo cha kikatili sana ulimwenguni. “Yeye,” Mtu aliye muhimu kuliko wote ulimwenguni. Unaona? Kwa nini? Hao watu wa kidini, dini iliyo kuu sana ulimwenguni, dini pekee iliyo ya kweli ulimwenguni, ilikuwa imesimama pale, ikimsulubisha Mungu yule yule ambaye Biblia yao ilisema angekuja.

<sup>235</sup> Kwa nini wao hawakuliona? Biblia inatuambia ya kwamba Mungu aliwapofusha hivi kwamba hawangeweza kuliona. Wao. . . Yeye alisema, “Ni nani wenu anayeweza kunihukumu kwamba Mimi nina dhambi?” Kwa maneno mengine, “Kama sikuwa nimefanya yale hasa yaliyotabiriwa kwamba nitayafanya, basi niambiieni.” *Dhambi* ni “kutokuamini.” Yeye alifanya sawasawa kabisa yale Mungu aliyomwambia, bali wao hawakuweza kuona jambo hilo.

<sup>236</sup> Sasa unapozungumza na watu, ni kama tu kutupa maji kwenye mgongo wa bata. Mnaona ninalomaanisha? Ni jambo la huzuni, unapooni taifa hili na watu hawa, namna wanavyofanya, wagumu sana na wamejaa dini! Lakini je! Roho si anatuambia jambo hilo? “Watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizua, na wasiopenda wale walio wema. Wangekuwa na mfano wa utauwa, lakini wangekana Nguvu za Injili.” Kasema, “Hao nao, jiepushe nao.”

<sup>237</sup> Haya sasa, hawa watu wa kimadhehebu wanalichanganya. Wanachukua utukufu wote na Nguvu, wanaziweka kule nyuma kwa mitume, na mengine yote huko katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Ni kama tu mwanadamu, kama nilivyosema hapo nyuma; mwanadamu daima anampa Mungu sifa kwa yale aliyotenda, akitazamia yale atakayokwishatenda, na kupuuza yale anayofanya sasa hivi. Hiyo ni kweli kabisa. Mwanadamu angali ni kitu kile kile.

<sup>238</sup> Kulikuwako na hao Wayahudi wamesimama pale, wakisema, “Mungu atukuzwe! Mbona,” kwenye sura ya 6 ya Yohana Mtakatifu, kasema, “Baba zetu walikula mana jangwani!”

Naye Yesu akasema, “Wao, kila mmoja wao, amekufa.”

<sup>239</sup> “Walikunywa maji kutoka kwenye ule Mwamba nyikani na kila kitu.”

<sup>240</sup> Yeye akasema, “Mimi Ndimi huo Mwamba.” Hiyo ni kweli. Amina. Akasema, “Lakini Mimi Ndimi Chakula cha Uzima kilichoshuka kutoka Mbinguni kwa Mungu, ule Mti wa Uzima kutoka mbali nyuma huko Edeni. Kama mtu akila Chakula hiki, yeye hatakufa kamwe; Nitamfufua tena katika siku za mwisho.” Na hata hivyo wao hawakuweza kuona jambo hilo! Hiyo ni kweli.

<sup>241</sup> Masihi Mwenyewe kabisa akisimama pale, akisema maneno yale yale yaliyokuwa moyoni mwao, na mambo kama hayo,



ikionyesha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, vile vile tu Masihi alivyopaswa kufanya!

<sup>242</sup> Nao wakimsimama pale huku wameweka mikono yao nyuma yao, na “A—ha! Haiwezekani. La, la. Yeye—Yeye—Yeye hakuja katika njia sahihi. Unaona, Yeye alikuja kutoka Bethlehemu. Na Yeye—Yeye si kitu ila ni mwana haramu. Na huyo ni Ibilisi akitenda kazi juu Yake. Tu—tunajua Yeye ana wazimu. Ana kichaa. Ana pepo.” Unaona? Macho yao kweli yalikuwa yamepofushwa juu ya jambo hilo, sasa.

<sup>243</sup> Lakini wao wanamtazamia nabii wao. Nao watampokea, watawapokea wawili. Hilo ni kweli.

<sup>244</sup> Sasa angalia, tena, sasa, pia, wakati Wayahudi hawa... Nitawapa mfano mwingine mdogo, ili kwamba mweze kutambua ya kwamba ni Wayahudi walio hapa sasa, upande huu wa Kunyakuliwa. Angalia jambo linalotukia. Limeonyeshwa pia kwa mfano... Hatutachukua wakati kulielezea, kwa sababu tumeishiwa—hatuna muda. Pia limeonyeshwa kwa mfano katika ninii ile... inayoitwa “taabu ya Yakobo.” Sasa angalia. Hawa Wayahudi hapa sasa wana-... Angalia. Loo! ni ninii...

<sup>245</sup> Ni—ni—nitachukua wakati mdogo tu hapa, unaona. Inanifanya niwe na wasiwasi wakati ninapoanza kuruka sehemu sehemu namna hiyo. Na... Mnaona? Angalieni. Nataka mwone jambo hilo. Nami ni—ni—ninaninii tu... Vema, Mungu atawaonyesheni hilo, nina hakika. Angalia.

<sup>246</sup> Yakobo alikuwa na ile haki ya mzaliwa wa kwanza. Sivyoy? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Lakini hakika alikuwa mdanganyifu kidogo kwa hilo. Unaona? Yeye alishuka akaenda na akamdanganya baba yake. Akamdanganya ndugu yake. Akafanya kila kitu. Lakini, hata hivyo, kihalali, moja kwa moja, aliipata, kwa sababu Esau alikuwa ameiiza. Lakini basi wakati anaposhuka na kwenda kule kufanya kazi kwa baba-mkwe wake, yeye anaweka hizo fito za mlubna majini, kuwafanya hao ng’ombe na kadhalika wenye mimba wazae ndama wenye madoadoa. Na, loo! mnajua kila kitu alichofanya cha namna hiyo, ili tu ku—kupata fedha. Sasa angalia, sasa. Yeye alifukuzwa kutoka kwa watu wake.

<sup>247</sup> Basi, ni mfano wa Wayahudi sasa. Yeye ni mpokonya-pesa. Mimi sijali anazipataje, atazipata. Atakuchuna ngozi ukiwa hai, kusudi azipate. Sasa, mnajua jambo hilo. Yeye ni bahili mdanganyifu, basi. Loo! usifanye biashara naye; yeye—yeye atakulangua, wee. Naam, bwana. Kwa nini? Hana budi kuwa namna hiyo. Hiyo ndiyo roho inayomtawala.

<sup>248</sup> Ni kama tu vile wale watengezaji, hawakuweza kulifahamu Neno hili, kwa sababu hiyo ilikuwa ni roho ya mwanadamu iliyotumwa kwao.

<sup>249</sup> Wakati wa tai ndio unaopata Neno na Ufunuo. Wote wanaofahamu jambo hilo, inueni mikono yenu, ili mimi... Ni

vizuri. Hilo ni sawa. Unaona? Ni vizuri. Sasa, unaona, kama unaweza kurudi nyuma hapa chini ya Mihuri hii, kama ikipata kuninii. . . Wakati itakapofunguliwa, unaweza kuona yale hasa Mungu anayofanya, yale aliyokwisha fanya, yale atakayofanya. Haya hapa, barabara kabisa.

<sup>250</sup> Na hiyo ndiyo sababu watu walitenda hivyo walivyotenda, kwa sababu hiyo ndiyo roho iliyobashiriwa kwa ajili ya wakati huo, kuwa juu yao. Hakuweza kufanya jambo lingine lo lote.

<sup>251</sup> Ninafikiri juu ya Yohana, Paulo, na hao wengine, hiyo Roho ya simba pale, s-i-m-b-a akisimama pale, Neno Lenyewe.

<sup>252</sup> Paulo alisimama imara na Neno hilo, na kusema, “Ninajua jambo hili, ya kwamba kutakuwako na ndugu wa uongo watakaoinuka kati yenu, kwenda huku nahuko. Na kile watakachounda, madhehebu na cho chote kile, kati yenu, na yale watakayofanya. Na jambo hio litaendelea hata siku za mwisho, na wakati wa kutisha.” Kwa nini? Yeye alikuwa ni nabii. Hilo Neno lilisimama ndani yake. Jinsi jambo hilo lingeshia, mbali kule nyuma; kasema, “Watu waongo kati yenu watainuka, nao wakinena mambo, na kuwavuta ndugu ambao ni wanafunzi.” Hao kabisa ndio yule mpinga-Kristo. Ilitukia vivyo hivyo kabisa.

<sup>253</sup> Angalia baada ya wao kuingia katika wakati ule wa giza wa ile dhiki. Ilikuwa ni nini? Hakuna jambo wangiweza kufanya. Rumi ilimiliki ninii. . . Yeye alikuwa na nguvu za kidini, na alikuwa na nguvu za kisiasa. Hakuna kitu wangeweza kufanya, ila ni kufanya tu kazi wapate kuishi, na kujitolea kuwa dhabihu. Ilikuwa ni ndama. Hivyo tu ndivyo wangiweza kufanya. Hiyo ndiyo Roho waliyokuwa nayo, Roho ya Mungu, yule ndama.

<sup>254</sup> Halafu, hawa hapa wanakuja wale watengenezaji, kichwa cha mwanadamu, mwerevu, mwenye akili; Martin Luther, John Wesley, na kadhalika, Calvin, Finney, Knox, na hao wengine. Hawa hapa wanakuja, na, walipokuja, walikuwa ni watengenezaji. Walitokea, wakitengeneza, wakiwatoa watu.

<sup>255</sup> Nao wakageuka moja kwa moja, kama tu vile hasa walivyofanya kule nyuma, na wakajiunga moja kwa moja kwake tena, kwenye utaratibu wao wa kimadhehebu, vile vile kabisa. Biblia ilisema hivyo. Yeye alikuwa ni “kahaba,” na halafu alikuwa na “makahaba,” wale mabinti, kweli kabisa.

<sup>256</sup> Na Mungu akasema, “Ni—nilimpa nafasi ya kutubu, naye hakutubu. Kwa hiyo nitamchukua yeye pamoja na watoto wake, na kuwatupa kule ambako wanastahili.” Naam. Sasa, hilo, Mungu alitamka jambo hilo, chini ya huu, unaona, chini ya ule Muhuri. Sasa huyo kahaba, alikuwa ndiye yeye pale. Tunaona ya kwamba Mungu anafanya jambo hilo, Naye atafanya hivyo. Nao hao, kila mmoja wao, ameelekea upande huo.

<sup>257</sup> Lakini, kwa wote ambao majina yao yameandikwa kwenye Kitabu cha Uzima, Mungu atawaita. Wataisikia.

“Kondoo wangu huisikia Sauti Yangu,” Yesu alisema. Jambo tu tunalopaswa kufanya ni kutoa mlio wa kondoo. Mbuzi hawaujui. Angalia. Lakini, unaona, mlio wa kondoo. “Kondoo Zangu huisikia Sauti Yangu.” Kwa nini? Sauti ni nini? Ninataka kuwaambia Sauti ni nini. Sauti ni—ni ishara ya kiroho.

<sup>258</sup> Yeye alimwambia Musa, “Kama hawataisikia Sauti ya ishara ya kwanza, watasikia Sauti ya ishara ya pili.”

<sup>259</sup> “Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu.” Wakati mambo haya yanapaswa kuwa yakitukia katika siku za mwisho, kondoo wa Mungu wanaitambua Hiyo. Naam, bwana. Unaona? Wao—wao wanaitambua. “Kondoo Wangu wananijua Mimi.” Unaona? “Mgeni hawatamfuata.” Hawawafuati hao wageni. Haina budi kuwa ni ishara iliyothibitishwa ya siku hiyo, nao wanaiona Hiyo. Sasa, basi angalieni.

<sup>260</sup> Sasa, Yakobo, alipokaribia sasa, muda si muda unajua, yeye alitamani kurudi (wapi?) katika nchi ya uenyeji wake.

<sup>261</sup> Loo! hivyo ndivyo Israeli walivyofanya hasa! Hivyo—hivyo. . . Hiyo ni Israeli. Yakobo ni Israeli. Alibadilishwa tu jina lake, mnajua. Unaona? Naye ni. . .

<sup>262</sup> Yeye alitoka pale, na akachukua pesa zote alizokuwa nazo, na ambazo angeweza kupata, na akazichukua vyo vyote alivyoweza, kutoka kwa jamaa zake ama ye yote yule mwingine. Kwa hiyo, kwa kudanganya, kuiba, kuhadaa, kwa njia yo yote aliyoweza kuzipata, alizipata. Unaona? Alizipata.

<sup>263</sup> Halafu basi wakati atakapoanza kurudi nyumbani, hana budi kusikia shauku ya kurudi nyumbani moyoni mwake. Lakini hapo alipoanza kurudi, alipokuwa akienda zake nyumbani, alikutana na Mungu, ndipo jina lake likabadilishwa. Unaona? Lakini, katika wakati huu, alikuwa ana hofu sana, kwa sababu alihofu Esau anakuja kumshambulia. Unaona?

<sup>264</sup> Basi—basi angalia, angalia hizo pesa, ile rai ya pesa. Kama tu vile Wayahudi watakavyojaribu kufanya agano hili na—na Rumi, unaona, katika rai yao ya fedha. Languale. Huyu Esau hakuhitaji fedha zake; wala Rumi. Ana utajiri mali wa ulimwengu mkononi mwake. Unaona? Lakini haikufaa kitu.

<sup>265</sup> Lakini tunaona sasa ya kwamba, kwamba Israeli, katika ule wakati wa taabu, wakati alipokuwa ni Yakobo, yeye alishindana na. . . ya kwamba yeye alipata Kitu fulani kilichokuwa halisi. Kulikuwa na Mtu aliyeshuka akaja. Yakobo akamkumbatia, na akakaa hapo. Na ninii—na ninii—Jamaa huyo akasema, “Sina budi kuondoka sasa. Kunapambazuka.” Loo! huko kupambazuka kwa siku! Unaona? Ilikuwa karibu kupambazuka.

<sup>266</sup> Lakini Yakobo akasema, “Si—sitakuacha. Wewe, huwezi kwenda. Nitakaa moja kwa moja na Wewe.” Unaona? “Nataka mambo yabadilishwe hapa.”

267 Hao ni wale mia na arobaini na nne elfu, lile kundi la watafuta-pesa, na mambo ya namna hiyo, watakapoona kitu cha kweli na kilicho halisi cha kushikilia. Huyo hapo amesimama Musa, na huyo hapo amesimama Eliya. Amina! Wao watapigana mweleka na Mungu mpaka mia na arobaini na nne elfu wa makabila ya Israeli wameitwa watoke papo hapo.

268 Hiyo ni kabla tu ya ule wakati wa ile Dhiki, unaona, (loo! jinsi linavyofurahisha) pia, “Taabu ya Yakobo.”

269 Hapa ndipo wale mia na arobaini na nne elfu wanapoitwa watoke. Wao, hao—hao wahubiri, hao manabii wawili, wanahubiri kama Yohana Mbatizaji. “Ufalme wa Mbinguni umekaribia. Tubuni, enyi Israeli!” Watubu nini? “Tubuni dhambi zenu, kutokuamini kwenu, na mumgeukie Mungu!

270 Sasa hebu na tukumbuke jambo fulani hapa. Mambo haya makuu yanayotukia, kwa maumbile, yametendeka hapo zamani. Katika aya hii ya 12 hapa, unaona, “Jua likawa jeusi kama gunia la singa. Sasa linganisha jambo hili.

271 Sasa, kumbukeni, hilo halitendeki kwa Mataifa. Ni kwa Israeli. Hebu niwaonyeshe. Sasa, kumbukeni, nilisema ni kule kuitwa kwa wale mia na arobaini na nne elfu. Unaona? Wakati huu sasa, ndipo ile Dhiki, ambayo itasababisha jambo hilo. Na hii inazungumzia yale yanayotukia katika Dhiki hii.

272 Sasa hebu na tufungue katika Kutoka 10:21-23. Na tuangalie hapa wakati. . . Kutoka ni wakati ambapo, bila shaka, Israeli walikuwa wanatoka, walipokuwa watolewe. Kutoka, sura ya 10, na aya ya 21, 23. Nimechangamka sana na kupaza sauti, ninapoandika mambo haya, hata wakati mwingine huenda nikayachanganya. Vema, Kutoka 10:21-23. Vema, sasa na twende, 21 na 23.

*Basi Bwana akamwambia Musa, Nyosha mkono wako kuelekea mbinguni, ili kuwe giza juu ya nchi ya Misri, giza watu wapapase-papase gizani.*

*Basi Musa akaunyosha mkono wake kuelekea mbinguni; basi kukawa na giza nene katika nchi yote ya Misri muda wa siku tatu; (Unaona?)*

*Sasa, hawakupata kuonana mtu na mwenziwe, wala hakuondoka mtu mahali alipokuwa muda wa siku tatu; lakini wana wa Israeli wote walikuwa na mwanga makaoni mwao.*

273 Angalia, ni vile vile kabisa, sasa hebu njoo upande huu, “Na jua likawa jeusi gunia la singa.” Unaona, kitu kile kile! Matukio haya ya maumbile, ilikuwa ni nini? Ati nini? Wakati maumbile yanapofanya hivi, imekuwa ni Mungu akiwaita Israeli. Unaona? Mungu anawaita Israeli watoke. Sasa, “Jua jeusi kama. . . nywele.” Sasa, Mungu alikuwa karibu na kuwakomboa Israeli pale, vema, kuwatoa katika mikono ya adui wao, ambaye

alikuwa ni Misri, wakati ule. Sasa, hapa, Yeye anawatoa katika mkono wa Roma, ambapo wao walikuwa wamefanya agano lao. Jambo lile lile linatukia. Hayo ni yale mapigo, wa—wakati ambapo mapigo yataingia.

<sup>274</sup> Yatalipiga kundi hili la Mataifa. Kama tungalikuwa na wakati, ningewaonyesha kitakacholipata kanisa hilo la Mataifa.

<sup>275</sup> Biblia ilisema, ya kwamba, “Yule—yule joka, Shetani, alimkasirikia (yaani, alimghadhabikia) huyo mwanamke (Myahudi, Israeli), naye akatoa maji toka katika kinywa chake, halaiki na umati wa watu, ambao walienda kufanya vita juu ya wazao waliosalia wa huyo mwanamke.” Ufunuo 13. Sasa, unaona hapo, tuna jambo hilo. Na hapo ndipo wakati ambapo Israeli inatuma ninii yake. . . namaanisha, Rumi inatuma jeshi lake dhidi ya uzao uliosalia wa yule mwanamke.

<sup>276</sup> Sasa angalia. Mara ya kwanza, katika mikono ya adui zao, hapo alipokuwa akiwatoa, jua liligeuka likawa sing- . . . jeksi kama singa. Sasa, hii ni mara ya pili, ule mwisho wa wakati wa ile Dhiki.

<sup>277</sup> Sasa, katika Danieli 12. Kama tungalikuwa na wakati, tungeweza kulisoma hilo. Katika Danieli, cha 12—kifungu cha 12. . . mlango wa 12, hasa. Danieli alisema, “Kila mmoja aliyekana ameandikwa katika Kitabu kile atakombolewa.” Sasa, kumbukeni, Danieli anazungumza sasa juu ya wakati huu ambapo haya. . . jambo hili linapaswa kutukia, wakati Israeli watakapokombolewa, wakati wa mwi—mwisho wa lile juma lao la sabini. Na hapo ndipo wanapopaswa kukombolewa. Sasa angalia. Hebu na tufungue Danieli 12 hapa, kwa muda kidogo tu.

*Basi wakati huo Mikaeli atasimama, yule jemadari mkuu, aliyesimama upande wa wana. . . u—upande wa wana wa watu wako (unaona, hao ni Wayahudi); na kutakuwa na. . . taabu, mfano. . . haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo; . . .*

<sup>278</sup> Sasa linganisha jambo hilo, vile vile hasa na alivyosema Yesu, Mathayo 24, “Kutakuwapo na dhiki kubwa ambayo haijatokea namna yake tangu kuwapo kwa taifa.” Angalia Muhuri wa Sita, unaona, jambo lile lile, wakati wa dhiki. Angalia.

*. . . tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo; na wakati huo watu wako. . . (Sasa, katika hili la sabini, sehemu ya mwisho ya ule mwaka wa saba). . . watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile.*

<sup>279</sup> Wale waliochaguliwa tangu zamani, unaona, ambao wameandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, watakombolewa wakati huo.

*Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, na wengine wapate uzima wa milele, na wengine aibu na kudharauliwa milele.*

*Sasa, ndipo walio na hekima watang'aa kama mwangaza wa mianga; na—na hao waongozao wengi kutenda haki watang'aa kama nyota milele na milele.*

280 Hilo, ndipo akaendelea, akamwambia Danieli “akifunge Kitabu kile,” kwa maana atastarehe katika kura yake mpaka wakati huo.

281 Sasa, unaona, haiteti tofauti yo yote kama unaishi ama unakufa. Unafufuka, hata hivyo. Unaona? Usiniii. . . Huko, kufa, si kitu kwa Mkristo. Yeye hafi, hata hivyo. Unaona?

282 Sasa, Danieli 12, ilisema ya kwamba kila mmoja aliyeonekana ameandikwa katika Kitabu kile atakombolewa.

283 Hapa, Mungu yuko karibu na kumkomboa mwanawe wa pili, Israeli, baada ya ile Dhiki. Unaona, mara ya pili, Israeli, ninii Wake. . . Israeli ni mwanawe. Mnajua jambo hilo. Israeli ni mwana wa Mungu, kwa hiyo Yeye atamkomboa hapa katika ule wakati wa Dhiki, kama vile vile tu kabisa alivyofanya kule Misri.

284 Sasa, hebu na tusimame hapa, tena, na—na tupate kitu kingine, basi, kabla hatujamalizia. Sasa angalia hapa. Manabii hawa wawili, angalia watakalofanya sasa, kama tu vile Musa na hao wengine walivyofanya nchini kule. “Nami nikapewa mwanzi. . .” Na aya ya 3 ya sura ya 11.

*Nami nitawaruhusu mashahidi wangu wawili, nao watatoa unabii siku elfu na mia mbili na sitini, hali wamevikwa magunia.*

*Hao ndio ile mizeituni miwili. . .*

285 Mnakumbuka jambo hilo, na Zerubabeli, na kadhalika, alikuwa ajenge lile hekalu.

*. . . na vile vinara viwili visimamavyo mbele za Mungu wa nchi.*

*. . . mtu ye yote. . . kuwadhuru, moto hutoka katika vinywa vya. . .*

286 Kumbukeni, kutoka katika kinywa cha Kristo unatoka upanga, Neno.

*. . . kuwala adui zao. Na mtu akitaka kuwadhuru, hivyo ndiyo impasavyo kuuawa.*

287 Sasa, tunajua, ule “moto.” Katika sura ya 19, kuhusu kule Kuja kwa Kristo, “upanga Wake unatoka katika kinywa Chake,” ambao ulikuwa ni Neno. Hiyo ni kweli? Neno! Loo! laiti ungalipata mambo haya sasa, kwa ajili ya ule Muhuri kesho usiku! Unaona, Neno ndicho kitu ambacho Mungu anatomia kuuwa adui Wake Nalo. Unaona?

288 Sasa angalia hapa. Wakati hawa manabii wanatabiri pale, wao. . . Kama mtu ye yote akiwatenda mabaya, akiwadhuru: “moto hutoka katika vinywa vyao,” Moto wa Roho Mtakatifu, Neno. Neno ni Mungu. Neno ni Moto. Neno ni Roho. Unaona? “Hutoka katika vinywa vyao.”

289 Mwangalie Musa. Hebu tuone kilichotoka katika kinywa chake. Wao, Israeli, walinini, jinsi walivyokuwa wakifanya pale, wale—wale. . . Ninamaanisha, Misri, wao walikuwa wakiwaudhi hawa Wayahudi. Musa. . . Vema, wao hawangewaruhusu kuondoka. Farao hangewaruhusu. Mungu aliweka maneno katika kinywa cha Musa. Unaona, ni mawazo ya Mungu yakiingia katika moyo wa Musa; yeye anaenda kule sasa kuyatamka, ndipo yanakuwa Neno. Akaunyosha mkono wake, akasema, “Na kuwe na nzi,” na hawa hapa inzi wakaja. Angalia hapa.

*Na mtu akitaka kuwadhuru, moto hutoka katika vinywa vyao na kuwala adui yao: . . .*

290 Unaona? Hilo hapo. Wao wanaweza kunena wanachotaka, na hicho hapo kinatokea, Amina!

*. . . mtu ye yote. . . kuwadhuru, hivyo ndivyo wao iwapasavyo kuuawa.*

291 Ndugu, Mungu anajitokeza jukwaani hapa!

*Hao wana amri ya—wana amri ya kuzifunga mbingu, ili mvua isinye katika siku za unabii wao. . .*

292 Eliya, yeye anajua jinsi ya kulifanya jambo hilo; aliishalifanya hapo zamani. Amina! Musa anajua jinsi ya kufanya jambo hilo; ameishalifanya hapo zamani. Hiyo ndiyo sababu ya wao kuhifadhiwa. Sasa. . . Amina!

293 Ningeweza kusema jambo fulani zuri sana papa hapa, lakini afadhali—afadhali niliache mpaka kesho usiku. Mnaona? Vema.

*. . . wana amri juu ya maji kuyageuza kuwa damu, na kuiipiga nchi kwa. . . mapigo, kila watakapo.*

294 Ni kitu gani? Ni nini kinachoweza kuleta vitu hivi ila Neno? Wao wanaweza kuyafanyia maumbile cho chote watakacho. Hili hapa. Wao ndio wanaouleta Muhuri huu wa Sita. Wao wanaufunua na kuufungua. Ni Nguvu za Mungu, kuyaingilia maumbile. Unaona, Muhuri wa Sita ni mchafuko wa maumbile kabisa. Mnalipata sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”] Huo hapo Muhuri wako. Ni akina nani wanaoutimiza? Ni hao manabii, ule upande wa pili wa Kunyakuliwa. Kwa Nguvu za Mungu, Neno la Mungu, wao wanayalaani tu maumbile. Wanaweza kutuma matetemeko ya nchi, kugeuza mwezi ukawa damu, jua linaweza kutua, ama cho chote, kwa amri yao. Amina!

295 Haya basi. Haya basi. Unaona? Unaona jinsi Mihuri hiyo ilivyofunguka, kule kwenye wakati wa kanisa, jinsi ilivyoonyesha wale wafia imani?

296 Na sasa hawa hapa manabii hawa wawili wamesimama hapa wakiwa na Neno la Mungu, kuyafanyia maumbile lo lote watakalo. Nao wanaitikisa dunia. Na inaonyesha ni nani hasa wanaofanya jambo hilo. Ni Musa na Eliya, maana hiyo hapo huduma yao imerudiwa tena, ni watu hao wawili. Loo! jamani! Mnaliona sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Unaona huo Muhuri wa Sita ni nini? Ni hao manabii. Sasa angalia. Usiliache likusonge roho. Lakini, angalia ni kitu gani kilichoufungua huo Muhuri, manabii! Unaona? Whiu! Amina! Ndio hayo.

297 Loo! tunaishi katika wakati wa tai, ndugu, tukielekea kwenye mawingu!

298 Wao waliufungua ule Muhuri wa Sita. Wana nguvu za kufanya hivyo. Amina! Huo hapo Muhuri wako wa Sita umefunguliwa. Unaona?

299 Sasa tunarudi nyuma moja kwa moja hapa, na Yesu alinena jambo hilo lingetukia. Huko nyuma kabisa katika Agano la Kale, huko nyuma katika Ezekieli, huko nyuma katika manabii wa kale, walisema lingetukia.

300 Na hapa ule Muhuri wa Sita umefunguka, watu wanasema, “Vema, hilo ni jambo lisilofahamika. Ni nini kilisababisha jambo hilo?”

301 Hii hapa siri yake, wale manabii, maana Biblia ilisema jambo hilo hapa. Wao wanaweza kufungua, wakati wo wote wao. . . . Wao wanaweza kufanya lo lote wanalotaka kwa maumbile. Nao wanafanya jambo lile lile walilofanya, amina, maana wao wanajua jinsi ya kulifanya. Amina! Utukufu!

302 Nilipoona jambo hilo, nilitoka tu kitini na nikaanza kutembea huku na huku sakafuni. Nikawaza, “Bwana, jinsi ninavyokushukuru, Baba wa Mbinguni!”

303 Huo hapo. Ndio wenyewe. Wao waliufungua huo Muhuri wa Sita. Amina! Waangalie, “Mtu akitaka kuwadhuru, moto hutoka katika kinywa chao,” Neno. Roho Mtakatifu alikuja juu ya mitume, unaona. “Moto ulitoka katika kinywa chao.”

304 Sasa angalia katika Ufunuo 19, tunaona jambo lile lile, “Na upanga mkubwa unatoka katika kinywa Chake,” Neno. Unaona? Kuja kwa Kristo. “Naye aliwaua adui Zake kwa Huo.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Sasa Yeye yuko njiani anakuja. Mwangalie sasa. Vema.

*Hao wana amri ya kuzifunga mbingu, ili mvua isinye katika siku za unabii wao: . . .*

305 Jamani, huko ni kuingilia maumbile! Sasa, ni kwa muda—muda gani mtu huyu, Eliya, alizifunga mbingu? [Kusanyiko linasema “Miaka mitatu na nusu.”—Mh.] Haya basi, sawa kabisa. Juma la sabini la Danieli, ile sehemu ya mwisho ya juma la



sabini ina muda gani? [“Miaka mitatu na nusu.”] Haya basi, sawa kabisa.

306 Musa alifanya nini? A—a—aligeuza ninii—maji yakawa damu. Alifanya miujiza hii yote ya namna hii, kama ile kabisa ambayo ilibashiriwa hapa chini ya Muhuri huu wa Sita. Na ndio hawa hapa, katika Ufunuo 11, wakifanya jambo lile lile. Amina!

307 Hizo hapo sehemu tatu mbalimbali katika Maandiko, papo hapo, zikishikamanisha kitu hicho pamoja. Huko ndiko kule kufunguliwa kwa Muhuri wa Sita. Ndio huo hapo kabisa! Amina! Utukufu! Sasa angalia.

*Hao wana amri ya kuzifunga mbingu, katika siku za unabii wao. Kusudi mvua isinyeshe: na . . . amri juu ya maji kuyageuza kuwa damu, . . . kuipiga nchi kwa mapigo, kila watakapo.*

308 Loo! jamani! Haya basi. Sasa fungueni papa hapa kwenye yale mapigo, unaona. Maumbile yote yameingiliwa, katika hili Pigo la Sita . . . ama Muhuri wa Sita, unapofunguliwa. Hilo ndilo lililotukia hasa. Sasa angalia. Ie . . .

309 Hapa, Mungu yuko tayari kumkomboa mwanawe, Israeli, katika namna ile ile ya dhiki ambayo alifanya wakati ule kule. Yeye alimtuma Musa kule na akawakomboa Israeli. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Naye alifanya mambo haya haya. Yeye alimtuma Eliya kwa Ahabu, na elfu saba wakatoka. Hiyo ni kweli? [“Amina.”] Yeye anawatuma moja kwa moja hapa tena, katika ule wakati wa ile Dhiki, na kuwaita wale mia na arobaini na nne elfu watoke.

310 Sasa, unaona, angalia, katikati ya Ufu- . . . ama katikati ya sura ya 6, ama lile Pigo la Sita . . . Muhuri, samahani, ule Muhuri wa Sita na Muhuri wa Saba. Sura ya 7 ya Ufunuo, kimahesabu, zinakaa pamoja vizuri.

311 Ni kama tu vile Marekani ilivyo nambari kumi na tatu; majimbo kumi na matatu iliyoanza nayo, nyota kumi na tatu kwenye bendera, koloni kumi na tatu, milia kumi na mitatu. Kila kitu ni kumi na tatu, kumi na tatu. Na inaonekana papa hapa katika mlango wa 13 wa Ufunuo. Hiyo ni kweli. Yeye ni kumi na tatu, na ni mwanamke.

312 Sasa, wakati Yeye alipokuwa anataka kumkomboa Mwanawe wa pekee, ambaye alikuwa ni Mwanawe wa pekee. Yakobo ni mwanawe; lakini huyu ni Mwanawe wa pekee. Mathayo 27, hebu tuone alilofanya pale. Mathayo, sura ya 27. Sasa, kumbuka, Mwanawe alikuwa amepigwa, na alikuwa amesumbuliwa, nao walikuwa wamemdhihakiki. Naye alikuwa sasa ameangikwa msalabani, saa tisa, alasiri ya Ijumaa Kuu. Karibu tu kutukia! Mathayo, sura ya 27 ya Mathayo, na a—aya ya 45, naamini ndiyo.

*Basi tangu saa sita palikuwa na giza juu ya nchi yote mpaka saa tisa.*

313 Sasa angalia vile tu hasa alivyofanya hapa nyuma sasa, katika jambo hili. Unaona?

*Nami nikaona, alipoifungua muhuri ya sita, tazama, palikuwa na tetemeko kuu la nchi; jua likawa jeusi kama gunia la singa, na mwezi—na mwezi wote ukawa kama damu,*

314 Weusi, giza! Misri; weusi, giza!

315 Mungu, akimkomboa Yesu msalabani, kabla tu Yeye hajamfufua katika ufufuo. Kwanza, giza; jua likatua katikati ya mchana, na nyota hazingetoa mwangaza. Siku mbili baadaye, Yeye alikuwa atamfufua katika ushindi mkuu.

316 Baada ya jua, na mwezi, na nyota, na kila kitu, kule Misri, yote haya kutukia, Yeye aliwakomboa Israeli akawapeleka kwenye nchi ya ahadi.

317 Hili hapa, katika wakati wa ile Dhiki, na hawa hapa wanasimama hao manabii ambao wana nguvu za Neno ambalo Mungu anawapa. Wanaweza kunena tu jinsi Mungu anavyowapa Neno.

318 Sasa, wao si miungu. Wao kwa kitambo. . . Kidogo, wao ni miungu, maana Yesu alisema walikuwa ni miungu. Alisema, “Mnawaita miungu, hao ambao Neno la Mungu liliwajilia.” Lakini, angalia, hao ndio wale ambao Mungu anaowaletea Neno. Na wakati anapolinena, linatukia. Hivyo tu.

319 Na huyu hapa akiwa na agizo kutoka kwa Mungu, kuipiga dunia, kila atakalo (loo, jamani), kuzifunga mbingu. Na anafanya hivyo. Kuna nini? Yeye yuko tayari kuwatoa wale mia na arobaini na nne elfu, kwa ajili ya ukombozi, kutoka kwenye Kitabu cha Ukombozi. Na hilo liko chini ya Muhuri wa Ukombozi, katika ule Muhuri wa Sita. Ndio huo, rafiki yangu mpendwa. Huo ndio ule Muhuri wa Sita; uliokuwa ni wa kisiri sana.

320 Hebu na tuchukue tu. . . Tuna dakika nyingine kumi. Hebu na tuchukue sehemu ndogo tu, unaona. Nina kama kurasa mbili tatu. Vema, ninaninii. . . Unaweza tu kuona, *hapa*. Nafikiri kuna kama. . . Kwenye huo, nafikiri nina kama kurasa kumi na tano zilizosalia bado, ningeweza kuziendea. Loo! kuna mengi sana juu ya jambo hilo! Jamani, unaweza tu kuendelea kutoka mahali pamoja mpaka mahali pengine! Lakini ninahofu tu nitawachanganya nikitawanya mengi kuliko kiasi. Na mimi si ninii. . . Siwezi kuyashikilia pamoja kama vile ingalinipasa kufanya.

321 Katika Isaya, hebu na tuchukue hili. Isaya, nabii, aliona huu Muhuri wa Sita umefunguliwa, na akanena habari zake; kama Huo ni muhimu, ama si muhimu. Unaona?

322 Vema, jambo lote, mpango wote wa ukombozi, uko chini ya Mihuri hii; Kitabu hiki chote.

323 Sasa kumbuka, tuliona Yesu aliuona. Hiyo ni kweli? Unaona? Yesu aliuona. Na sasa tunaona wengine ambao waliuona. Tunauona ukionyeshwa kwa mfano katika—katika Yakobo. Tunauona umeonyeshwa kwa mfano kule Misri. Tunauona umeonyeshwa kwa mfano pale msalabani.

324 Sasa hebu na turudi katika Isaya. Nina manabii wengi zaidi walioandikwa hapa, pia. Hebu tuninii tu. . . Ninalipenda hili, hili la Isaya. Hebu na turudi hapa kwa Isaya, mlango wa 13 wa Isaya. Ninapenda. . .

325 Isaya ni—ni Biblia nzima, kwa Chenyewe, unajua. Je! ulijua jambo hilo? Unaona, Isaya anaanza na uumbaji; katikati ya Kitabu yeye anamleta Yohana; na mwishoni analeta ule Utawala wa Miaka Elfu. Na kuna vitabu sitini na sita katika Biblia, na sura sitini na sita katika Isaya. Ni itafaki kamili, Yenyewe.

326 Angalia, sura ya 13 sasa, ya—ya Isaya. Hebu na tuanzia hapa kwenye aya ya 6.

*Pigeni kelele za hofu; maana siku ya BWANA i karibu; itakuja kama maangamizi yatokayo kwa Mwenyezi Mungu.*

327 Angalia Muhuri huu wa Sita ukifunguliwa hapa sasa. Moja kwa moja huku nyuma, miaka mia saba na kumi na tatu kabla Kristo hajaja, Naye amekaa miaka elfu mbili, hiyo ingekuwa kama ninii saba. . . kama miaka elfu mbili mia saba iliyopita. Isaya aliuona Muhuri huu ukining'inia pale. Vema.

*Kwa sababu hiyo mikono yote italegea, na moyo wa kila mtu utayeyuka.*

328 Yesu alisema nini? “Na kwa sababu ya kuongezeka kwa maasi, u—upendo wa wengi utapoa basi.” “Watu watakuwa wakivunjika moyo, kwa hofu; bahari ikivuma.” Unaona, mioyo ya watu italegea.

*Nao watafadhaika; watahikwa na utungu na maumivu; watakuwa na utungu kama mwanamke aliye karibu na kuzaa; watakodoleana macho; nyuso zao zitakuwa za aibu.*

329 Angalia jambo hilo tena hapa, loo! “nyuso zao, aibu.” Hatuna budi kufikia jambo hilo, hivi punde tu. Nitashikilia jambo hilo, unaona.

*Tazama, siku ya BWANA inakuja, siku kali, ya hasira na ghadhabu kuu, ili iifanye nchi kuwa ukiwa, naye atawaharibu watu wake, wenye dhambi.*

330 “Nchi,” yaani yote, hiyo yote—unaona. Angalia.

*Maana nyota za mbinguni na matangamano havitatoa nuru yake; jua litatiwa giza wakati wa kujaa kwake, na mwezi utaacha nuru yake isiangaze.*

*Nami nitaadhibu ulimwengu kwa sababu ya ubaya wao, na hatia, na uovu kwa sababu ya hatia yao; nami nitaikomesha faha- . . .*

331 Si—sijui jinsi ya kuendeleza herufi zake, faha- . . . [Kusanyiko linasema, “Fahari.”—Mh.] Siwezi kulitamka, unaona.

*. . . yao wenye kiburi; nami nitayaangusha chini majivuno yao—yao walio wakali—wakali.*

332 Unaona, hapo, ni kitu kile kile kabisa, Isaya aliona jambo lile lile ambalo Yesu alilinenana habari zake. Ambalo Muhuri wa Saba unafunua. Wakati Yeye anaisafisha nchi kwa ile dhiki, huo ni wakati wa ile Dhiki, huu Muhuri wa Sita. Naam, yeye alikuwa ni nabii, naye alijulishwa Neno la Mungu. Hiyo ni miaka elfu mbili mia saba iliyopita.

333 Kweli! Ninataka tu kusema jambo hili. Ulimwengu mzima, kama vile Isaya hapa, “utungu kama mwanamke aliye karibu na kuzaa,” viumbe vyote vinaugua. Huku kuugua kote na kushikwa na utungu ni kwa ajili gani? Kama mwa—mwa—mwanamke aliye karibu na kuzaa; dunia yenyewe, maumbile.

334 Mbona, mji huu hapa, hebu na tuchukue mji wetu wenyewe; wakati, vilabu vya pombe, na umalaya, na uchafu, na vinyaa, kama mji mwingine wo wote!

335 Mbona, ninaamini Mungu angeona ni afadhali, akiiangalia jinsi alivyoiumba, miaka elfu iliyopita. Wakati Ohio ulipotiririka, hawakuwa na mabwawa na mafuriko. Hawakuwa na dhambi huko bondeni. Nyati walienda huku na huko hapa, na—na maskini Cherokee wa zamani za kale waliwawinda na kupata riziki nzuri. Hapakuwapo na shida, hata kidogo.

336 Lakini, mwanadamu akaingia, hapo ndipo dhambi inapoingia. Watu walipoanza kuongezeka juu ya uso wa dunia, ndipo dhambi na uhalifu vilipoanza. Hiyo ni kweli, daima ni mwanadamu. Jamani, ninafikiri ni aibu!

337 Nilikuwa nimesimama, juzijuzi, katika nchi ya wenyeji wangu kule, sasa kule Arizona. Na—nami nikasoma, nilipokuwa mtoto, juu ya Geronimo, na—na Cochise, na hao Waapache wa kale. Maana, niliwahubiria kule. Watu wazuri! Na baadhi ya watu wazuri sana unaotaka kukutana nao, ni hao Wahindi Waapache.

338 Na basi nikaenda kule—kule Tombstone, ambako wana tunu zote za kale na vitu vingi vingi kutokana na vita. Nami nikaangalia kwenye . . . Wao daima, unajua, daima walimhesabu Geronimo kama—kama haini. Kwangu mimi, alikuwa ni Mmarekani halisi. Kweli kabisa! Yeye alikuwa tu anapigania

haki zake, kama mtu ye yote yule angalifanya. Hakutaka uchafu huo katika nchi yake. Basi angalia jinsi ilivyo sasa; kuwafanya watoto wake, mabinti wake, kuwaingiza katika umalaya, na mengine yote; nao wazungu waliingia kule. Mzungu ni mwovu.

<sup>339</sup> Mhindi alikuwa ni mtunzaji. Yeye alikuwa—alikuwa ni mtunzaji. Yeye angeenda zake na kumwua nyati, kabila lote linakula kila kitu kilichosalia kwake. Walitumia ngozi kutengeza nguo na mahema, na vitu vinginevyo. Naye mzungu anakuwaja na kuwaua, kulenga shabaha; jamani, ni aibu sana!

<sup>340</sup> Nilisoma makala fulani gazetini, ambapo, huko Afrika, mahali pale mashuhuri palipojaa wanyama pori! Wanawaruhusu jamaa hawa, akina Arthur Godfrey na kadhalika, kuenda kule, wanawapiga risasi hawa tembo na wanyama wengine, wakiwa kwenye helikopta na vitu kama hivyo. Picha ya maskini tembo wa kike mzee akijaribu kufa, na hayo machozi, kitu kama hicho, yakitiririka usoni mwake. Na dume wawili wakijaribu kumshikilia, kumfanya . . . Mbona, ni dhambi. Huo si uwindaji.

<sup>341</sup> Ninaposimama huko mbugani, na kule ninakowinda na vitu kama hivyo, na kuona ambapo hao wazungu wawindaji wanapokuja kule na kuwaua kulungu, kukata miguu yake ya nyuma. Na wakati mwingine wanawaua maskini majike manane ama kumi wa kulungu, na kuwaacha wamezagaa pale. Ndama wao wakikimbia huku na huko, wakijaribu kumtafuta mama yao. Nawe unataka kuniambia huo ni uwindaji? Hayo ni mauaji ya kinyama, katika kitabu changu.

<sup>342</sup> Natumaini Canada haitafunguliwa njia zo zote kamwe, kadiri nikali hai, kuwazuia hao Wamarekani wahuni kuingia kule. Hiyo ni kweli. Huo ni uwindaji haramu sana niliopata kuona maishani mwangu.

<sup>343</sup> Sasa, si wote. Kuna watu halisi, wa kweli, lakini, utakayempata, ni mmoja kati ya elfu.

<sup>344</sup> Wanapiga risasi cho chote wanachoweza kuona, vyo vyote watakavyo. Hiyo ni kweli. Huyu ni muuaji. Hiyo ni kweli. Yeye hana huruma. Naye anawapiga risasi, si katika msimu wake.

<sup>345</sup> Vema, huko juu Alaska kule, nilikuwa kule pamoja na mmoja wa hao magaidi. Akasema, “Nilichukua . . . Ningeenda huko sasa, na kukupata kundi zima la hao kulungu wakubwa ama . . . si kulungu wakubwa, bali ni kongoni wamezagaa pale; wamepigwa risasi za bom-bom zenye kipimo cha hamsini kwenye pembe zao, ambapo hawa marubani wa Kimarekani sehemu zile, kule Alaska, wakiwapiga kwa bom-bom, kutoka kwenye ndege, kundi la kongoni.” Hayo ni mauaji halisi ya kinyama.

<sup>346</sup> Wao walijua, kila wakiua nyati hao, wangempata Mhindi. Yeye angekufa kwa njaa. Hiyo ndiyo sababu Cochise alilazimika kujisalimisha; ninii wake, wanawe wote wa kifalme, na hao wengine wote, watoto wake, na watu wake wote, walikuwa

wakifa kwa njaa. Wao walienda kule wakiwa na lundo la mzungu mikubwa ya hao, Buffalo Bill na hao watu wa nchi tambarare, na kuwaua hao nyati wote, arobaini, hamsini, katika alasiri moja. Wanajua, watakapowaangamiza hao, wamemwangamiza Mhindi. Loo! jamani! Ni waa katika bendera, jinsi walivyowatendea hao Wahindi. Unaona.

<sup>347</sup> Lakini kumbukeni, Biblia ilisema, “Saa imewadia ambapo Mungu atawaangamiza hao wanaoingaiza dunia.” Na ulimwengu mzima!

<sup>348</sup> Angalia hayo mabonde. Nilikuwa nimesimama juu kule, juzijuzi, nikiangalia kwenye bonde kule Phoenix. Nikaenda huko South Mountain, mimi na mke wangu tulikuwa tumeketi kule juu, na tukaangalia kule chini Phoenix. Nami nikasema, “Hilo si ni jambo baya sana?”

Mke wangu, “Baya?” Una maana gani?”

<sup>349</sup> Nikasema, “Ile dhambi. Na ni uzinzi mngapi, na unywaji pombe, na kulaani, na Jina la Bwana kutumiwa bure, katika bonde lile kule; lenye watu wapatao mia moja na—na arobaini, hamsini elfu, ama labda watu laki mbili, kwenye bonde lile!”

<sup>350</sup> Nikasema, “Miaka mia tano iliyopita, ama elfu moja, hakukuwako na kitu ila mipungate, mikonge, na mbwa mwitu wakikimbia huku na huko kwenye mto wa changarawe kule, katika mi—mikondo ya maji.” Ndipo nikasema, “Hivyo ndivyo Mungu alivyoifanya.”

<sup>351</sup> Lakini, mwanadamu akaingia. Alifanya nini? Aliijaza nchi sana na uchafu. Mitaa imejaa chuki. Taka, ninii... Na mito imechafuliwa kwa—kwa taka. Wao wasingeninii... Mbona, afadhali usinywe fundu moja la hayo maji; ungepata cho chote. Unaona? Hebu angalia jambo hilo. Si hapa tu, bali, kila mahali ulimwenguni, hiyo imechafuliwa!

<sup>352</sup> Na ulimwengu, viumbe, (Mungu na aturehemu!) ulimwengu mzima... na utungu wa kuzaa. Ulimwengu unajaribu, “unaugua,” Isaya alisema. Kuna nini? Uko katika... unajaribu kuzaa ulimwengu mpya, kwa ajili ya ule Utawala wa Miaka Elfu, ambapo ninii yote...?... Unajaribu kuzaa ulimwengu mpya, kwa ajili ya watu wapya ambao hawatatenda dhambi na kuuchafua. Hiyo ni kweli. Unaugua. Hiyo ndiyo sababu ile—ile... Sisi tunaugua, Kristo, kumzaa Bibi—arusi. Kila kitu kinaugua na kutaabika. Unaona, kuna kitu karibu kutukia.

<sup>353</sup> Na Pigo hili la Sita linauachilia. Ndugu, tetemeko la nchi linapasuka, na nyota zinatetemeka, volkeno zitatokea, na dunia itajitengeneza upya. Lava mpya italipuka kutoka katikati ya dunia. Nayo itavunjikavunjika, na itazunguka na kuzunguka na kuzunguka, hapo itakapozunguka—zunguka huko.

<sup>354</sup> Nami nawaambia, asubuhi moja wakati Yesu na Bibi—arusi Wake watakaporudi duniani, kutakuwako na paradiso ya

Mungu kule. Hao, loo! jamani, hao mashujaa wa kale wa vita, watakapotembea kule pamoja na marafiki wao na wapendwa wao. Nyimbo za sifa zitajaa hewani, za jeshi la Malaika. “Loo! ilikuwa vema, mtumishi wangu mwema na mwaminifu. Ingia katika furaha ya Bwana, ambayo imeandaliwa kwa ajili yako, kama ile uliyopaswa kuwa nayo kule nyuma kabla Hawa hajasababisha jambo la dhambi kuanza. Amina! Whiu! Naam.

<sup>355</sup> Muhuri wa Sita utafanya jambo fulani. Naam, bwana. Hakika ulimwengu mzima unaugua na kuumia, kwa ajili ya ule wakati wa Utawala wa Miaka Eflu!

<sup>356</sup> Sasa, ule uliopo sasa umelowa sana katika uchafu! Jambo ambalo nilihubiri hapa, si muda mrefu uliopita, naamini, nilihubiri maskanini, *Ulimwengu Unavunjika Vipande-vipande*. Hiyo ni kweli kabisa. Angalia kile kinachovunjika vipande-vipande ulimwenguni. Angalia, kila kitu kinaanguka, kutoka kwake. Bila shaka, kinaanguka. Hakina—hakina budi kuanguka vipande-vipande. Naam, bwana.

<sup>357</sup> Angalia, fremu yake! Hebu niwaonyeshe sababu gani ulimwengu hauna budi kufanya hivyo. Fremu ya dunia hii, chuma, na shaba, na lupa na madini ya dunia hii, vimechimbuliwa toka kwake, fremu yake, kwa ajili ya vita na viwanda, mpaka uko tu karibu. . . Vema, hatujapata kuwa na tetemeko la nchi mpaka juzijuzi, katika sehemu hii ya nchi; juzijuzi tu hapa, unaona, St. Louis na kule chini kote. Dunia inakuwa nyembamba sana. Wametoa kila kitu ndani yake. Unaona?

<sup>358</sup> Siasa zake zimechafuka sana, hata ni vigumu kumpata mtu mwaminifu kati yao, unaona, utaratibu wake. Uadilifu wake ni duni sana, hauna uadilifu hata kidogo. Ni hivyo tu. Unaona? Hakika. Dini yake imeoza. Naam, bwana.

<sup>359</sup> Ni wakati wa ule Muhuri wa Sita, hivi karibuni sana, kuanza kufunguliwa. Na wakati utakapofunguliwa, loo! jamani, ulimwengu unakwisha! Bibi-arusi ameondoka tayari, yeye tayari. . . Malkia tayari amekwenda kupachukua mahali pake; Ameolewa tayari sasa, na yule Mfalme, wakati mambo haya yanapoendelea. Nao mabaki ya Israeli wametiwa muhuri na wako tayari kuondoka, ndipo maumbile yanaachilia. Loo! ni wakati wa jinsi gani!

<sup>360</sup> Angalia aya ya mwisho ya Muhuri wa Sita, ulipofunguliwa. Wale waliokuwa wamecheka kuhubiriwa kwa Neno, kuhubiriwa kwa Neno lililothibitishwa la Mungu aliye hai; wakati hao manabii walipokuwa wamesimama pale na kufanya miujiza, wakalifunga jua, na vitu vingine vyote, na kote kote katika wakati. Unaona, “Waliililia miamba na milima iwasitiri,” unaona, kuwasitiri mbele ya Neno walilokuwa wamelicheka, maana wao walimwona Yeye akija. “Tusitirini mbele za hasira ya Mwana-Kondoo.” Yeye ni Neno. Unaona? Wao walikuwa

wamelicheka Neno. Na hili hapa Neno, limefanyika mwili. Nao wakalidhihaki; waliwacheka, wakawafanyia mzaha. Nalo Neno lililofanyika mwili lilikuwa limekuja!

<sup>361</sup> Kwa nini wao hawakutubu? Hawakuweza. Waliishachelewa sana, wakati huo. Kwa hiyo, wao walijua ile, ile adhabu. Walilisia. Waliketi katika mikutano kama hii na kujua habari Zake. Nao walijua ya kwamba mambo ambayo hao manabii, walikuwa wamebashiri, yalikuwa yakiwakazia macho moja kwa moja usoni, lile jambo ambalo walikuwa wamelikataa. Walikuwa wamekataa rehema kwa mara ya mwisho.

<sup>362</sup> Na mtu unapokataa rehema, hakuna kitu kilichosalia ila hukumu. Wakati unapoikataa rehema; wazia tu jambo hilo.

<sup>363</sup> Nao walikuwa ndio hao hapo. Hawakuwa na mahali pa kwenda, hakuna mahali pa kukimbilia. Na Biblia ilisema hapa, “Waliita ninii...Wakalilia miamba na milima, wakisema, “Tuangukieni, na tusitirini na uso—uso wa...na hasira ya Mwana-Kondoo.” Walijaribu kutubu, bali Mwana-Kondoo alikuwa amekuja kuwadau walio Wake, unaona. Nao waliililia miamba na mlima. Wakaomba, bali maombi yalikuwa yamechelewa sana.

<sup>364</sup> Ndugu yangu, dada, wema na rehema za Mungu, zilizotolewa kwa watu. Wakati, Israeli walikuwa wapofushwa kwa ajili ya jambo hili, kwa jambo hili hapa, yapata miaka elfu mbili, la kutupa sisi nafasi ya kutubu. Je! umekataa hiyo rehema? Umeikataa? Umeikataa Hiyo?

<sup>365</sup> Wewe ni nani, hata hivyo? Ulitoka wapi? Na unaenda wapi? Hungeweza kumwuliza daktari, hungeweza kumwuliza mtu ye yote ulimwenguni, wala hakuna kitabu ungaliweza kusoma, ambacho kingeweza kukwambia wewe ni nani, unatoka wapi, na unakwenda kuninii, ila Kitabu hiki.

<sup>366</sup> Sasa, unajua, bila wewe kuwa na ile Damu ya Mwana-Kondoo kusimama mahali pako, unaona unakoelekea. Kwa hiyo, kama—kama Mungu alifanya jambo hilo kwa ajili yako, jambo dogo sana tungaliweza kufanya lingekuwa ni kukubali yale Yeye aliyokwisha kufanya. Hayo ndiyo tu anayotutaka tufanye.

<sup>367</sup> Na juu ya msingi wa jambo hili, kama nikienda umbali wo wote zaidi, itanibidi kuja moja kwa moja kwenye lile Pigo, yote hayo, ibada ya kesho usiku. Na sasa siwezi kufanya jambo hilo, siwezi kwenda mbele zaidi. Nimechora hapa chini, msalaba, “simama hapa,” unaona. Kwa hiyo, basi, sina—sina budi kungojea hadi kesho.

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kidogo.

<sup>368</sup> Kama hujaninii, rafiki yangu mpendwa, huja—hujakubali upendo wa Mungu huyu ambaye ninanena habari Zake! Kama hujaninii...Sikiliza jambo hili kwa makini sasa. Kama



hujakubali upendo Wake na rehema, huna uje usimame mbele ya hukumu Zake na hasira.

<sup>369</sup> Sasa, wewe, usiku wa leo, uko mahali pale pale ambapo Adamu na Hawa walikuwa katika Bustani ya Edeni. Una haki. Wewe ni mtu mwenye hiari ya kujichagulia. Unaweza kwenda kwenye ule Mti wa Uzima, ama unaweza kuchukua mpango wa hukumu. Lakini, leo, wakati ungali una akili, katika akili zako timamu, na una afya ya kutosha ku—kuamka na kulikubali, mbona usifanye jambo hilo kama hujalifanya bado.

<sup>370</sup> Je! kuna watu hao humu ndani ambao hawajaninii, bado, hawakufanya hivyo? Kama hivyo ndivyo ilivyo, tafadhali inua tu mkono wako, useme, “Niombe, Ndugu Branham. Sasa ninataka kufanya jambo hilo. Sitaki hili lije.” Sasa kumbukeni, enyi marafiki. . . Mungu awabariki. Ni vizuri. Nina. . .

<sup>371</sup> Haya si mawazo yangu juu ya Hili. Mimi—mimi. . . Hivi sivyo nimekuwa nikiwazia; kwa jumla hili linatoka kwangu. Kwa hiyo anisaidie, Roho Mtakatifu anajua jambo hilo. Nanyi ngojeni, Bwana akipenda, kesho usiku, ninataka kuwaonyesha siri ambayo imekuwa ikiendelea wakati wote, papa hapa katika mkutano huu. Nina shaka sana kama mmewahi kuliona ama hamjaliona, mnaona, ja—jambo lililotukia. Limekuwa ni jambo ambalo limekuwa papa hapa mbele yenu. Nami nimeangalia, kila usiku, hili, lipate kutokea, mtu fulani apate kusema, “Ninaliona.” Mnaona?

<sup>372</sup> Usilikatae, tafadhali, nakuomba; kama wewe si Mkristo, kama wewe—kama wewe huko chini ya ile Damu, kama hujazaliwa mara ya pili, ukajazwa na Roho Mtakatifu.

<sup>373</sup> Kama hujamkiri Ye—Yesu Kristo hadharani, kwa kubatizwa katika Jina Lake, kushuhudia mauti Yake, kuzikwa na kufufuka Kwake, ya kwamba umekubali, maji yako tayari. Wao wanangojea. Nguo ndefu zinatolewa hapa, na kila kitu kiko tayari.

<sup>374</sup> Kristo amesimama akiwa tayari, akiwa na mkono ulionyoshwa, kukupokea. Katika saa moja tangu sasa, rehema hiyo huenda isitolewe kwako. Huenda ukaikataa kwa mara ya mwisho; haitaugusa moyo wako tena. Wakati unaweza, wakati unaweza, mbona usifanye jambo hilo? Sasa wakati. . .

<sup>375</sup> Ninajua njia ya kawaida, na ya mazoea, ni kuwaleta watu madhabahuni. Tunafanya jambo hilo, na hilo ni sawa kabisa. Wakati huu, tumesongamana sana hapa ndani, kila mahali kuzunguka madhabahu, mpaka singeweza kufanya jambo hilo.

<sup>376</sup> Lakini ningetaka kusema jambo hili. Katika siku za mitume, wao wanasema, “Wote walioamini walibatizwa.” Unaona? Kama tu unaweza, kweli, ndani ya moyo wako! Kila kitu kiko hapa hapa. Si—si msisimko, ingawa msisimko hufuatana nalo. Ni kama tu nilivyosema, kuvuta sigara na kunywa pombe si dhambi; ni tunda la dhambi; inaonyesha wewe huamini.

Unaona? Lakini wakati unapoamini kweli katika moyo wako, nawe unajua jambo hilo juu ya msingi wa ninii, hapo mahali unapoketi hapo, likubali kwa moyo wako wote, kitu fulani kitatukia papo hapo. Kitatukia.

<sup>377</sup> Ndipo unaweza kusimama kama shahidi wa jambo hilo, ya kwamba jambo fulani limetukia. Ndipo unaenda kwenye maji, useme, “Nataka kulionyesha kusanyiko, nataka kuthibitisha, ninataka kuufanya ushuhuda wangu uthibitike, ya kwamba nitachukua nafasi yangu pamoja na Bibi-arusi. Ninasimama hapa sasa nipate kubatizwa.”

<sup>378</sup> Ninajua ya kwamba kuna wanawake wengi duniani usiku wa leo, wanawake wazuri, lakini mimi natamani sana kumwona mmoja. Kuna mmoja wao ambaye ni mke wangu. Yeye anaenda nyumbani nami. Yeye hakuwa mke wangu, kwanza; lakini jinsi alivyofanyika mke wangu, yeye alichukua jina langu.

<sup>379</sup> Yeye anakuja. Kuna wanawake wengi, makanisa, ulimwenguni, lakini Yeye anakuja kwa ajili ya Mke Wake. Yeye anaitwa kwa Jina Lake. “Hao walio katika Kristo Mungu atawaleta pamoja Naye.” Tunaingiaje ndani Yake? “Kwa Roho Mmoja sisi sote tumebatizwa katika Mwili mmoja.”

<sup>380</sup> Sasa wakati tukiomba, wewe omba, pia. Ndani ama nje, kuna makundi makubwa ya watu vyumbani, huko nje, wanaosimama huko, huko nje barabarani. Lakini sasa wakati—wakati mnaninii. . . Hatuwezi kuwaita hapa madhabahuni. Lakini, moyo wako, ufanye kuwa ndio madhabahu. Na moja kwa moja moyoni mwako, useme, “Bwana Yesu, ninaamini jambo Hili. Nilisimama hapa nje kwenye hewa ya usiku. Nimesongwa roho katika chumba hiki kidogo. Nimeketi hapa ndani, miongoni mwa watu hawa. Si—si—si—si—sitaki kuwa. . . Siwezi kukosa; siwezi kufanya jambo hilo.”

<sup>381</sup> Kila kitu, kama nilivyowaambia jana usiku, na, kwa hiyo na anisaidie, Bwana anajua ninasema Kweli. “Sisemi uongo,” kama vile alivyosema Paulo. Ono lile, ama cho chote kile lilichokuwa; nilisimama kule, niliangalia, na kuwashika hao watu ambao wamekwisha ondoka, halisi tu kama ninavyosimama papa hapa. Usilikose, maskini ndugu yangu ama dada, usilikose. Ninajua umesikia mahubiri, umesikia jambo *hili, lile*, na hadithi nyingi, yote hayo. Lakini hebu. . . sikiliza tu. Kwangu mimi, hii ni. . . Ninajua ni Kweli, unaona. Wewe ninii tu. . . Si—siwezi kulifanya dhahiri zaidi, unaona. Usilikose. Yote ni yako.

Sasa na tuombe.

<sup>382</sup> Bwana Yesu, hapa mbele yangu kuna sanduku la vitambaa ambavyo vinawakilisha watu walio wagonjwa. Ninapoviombea, nikiviwekea mikono, kama Biblia ilivyosema, “Walichukua kutoka katika mwili wa Paulo, vitambaa na lesa, pepo wachafu wakawatoka watu, na ishara kuu zilifanywa.”

383 Kwa sababu, wao walimwona Paulo, kwamba wao walijua Roho wa Mungu alikuwa ndani yake. Wanajua ya kwamba—ya kwamba alikuwa ni mtu asiye wa kawaida, yaani, mambo ambayo alinena juu yake, kuhusu Neno. Yeye angeenda na kuchukua neno la kale la Kiebrania la kanisa la Kiebrania, na kulifanya hai, na kuliweka katika Kristo. Wao walijua Mungu alikuwa ndani ya mtu huyo. Ndipo wakamwona Mungu akitenda mambo ya ajabu na makuu kupitia kwake, akitabiri mambo na yangetukia namna hiyo, nao wanajua ya kwamba yeye alikuwa ni mtumishi wa Mungu.

384 Bwana, naomba ya kwamba Wewe utawakubali watu hawa kwa ajili ya heshima yao ya Neno, na uwaponye kwa ajili ya Yesu. Hapa nje katika wasikilizaji, Bwana, kuna watu walioketi, kama tu ilivyokuwa kwa wale waliomsikiliza mtume Petro kwenye ile Siku ya Pentekoste. Jinsi alivyokwenda nyuma kwenye Neno, na kulichukua Neno! Naye akasema, “Yoeli alisema, katika siku za mwisho mambo haya yatatukia. Na hili ndilo lile.” Na wale elfu tatu wakaamini Hilo, na wakabatizwa.

385 Na, Baba, leo tunasimama hapa kwa neema Yako. Na si kwa sababu kwamba—kwamba ni watu maalum, lakini ni kwa sababu (kama tu zile siku za simba, ama ndama, ama mwanadamu) ni wakati wa tai. Ndio upako wa wakati huu. Ni wakati tunaishi. Ni kutenda kwa Roho Mtakatifu kwa ajili ya wakati huu hasa, kuthibitisha ya kwamba Yesu si mfu. Mambo ambayo alisema ya kwamba angefanya kabla tu ya zile Nuru za jioni kuzimika, nasi hapa tumekuwa tukimwona Yeye akifanya hivyo, moja kwa moja tu njiani. Tumeona Hiyo ikishuka katika utafiti wa kisayansi na picha Yake ikapigwa; ile Nguzo kuu ya Moto Ambaye aliwaongoza wana wa Israeli; Ambaye alikutana na Paulo njiani.

386 Nasi tunajua, Nguzo ii hii ya Moto ambayo ilimwongoza Musa kule nyikani, kwa Nguzo ile ile ya Moto yeye aliandika Vitabu kadha wa kadha vya Biblia, kwa maana Yeye alikuwa ametiwa upako kwa Neno.

387 Nguzo ii hii ya Moto ilipokuja juu ya Paulo, akienda zake Dameski, aliandika Vitabu vingi vya Biblia, vinavyoitwa Neno la Mungu.

388 Na sasa, Bwana, Nguzo ile ile ya Moto, kwa ushuhuda wa thibitisho la Neno, na kwa utafiti wa sayansi, tunaiona hapa ikilifunua Neno la Bwana.

389 Mungu, wajalie watu waamke upesi, Bwana, upesi! Hao ambao majina yao yameandikwa katika Kitabu cha Uzima; wakati Hili litakapomulika njiani mwao, naomba waone. Kama maskini yule mwanamke mwenye sifa mbaya pale kwenye kisima siku ile, yeye alitambua upesi, naye alijua Hayo yalikuwa ni Maandiko.

<sup>390</sup> Na sasa, Baba, naomba ya kwamba wote watakaokupokea Wewe wakati huu, mioyoni mwao, wataamua kwa milele, katika saa hii, ya kwamba wamemalizana na dhambi; ya kwamba wataamka na kufanya matayarisho sasa kwa ajili ya kukiri mbele ya watu, kuhusu ubatizo wa katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zao; kuonyesha ya kwamba wao wanaamini ya kwamba Mungu amewasamehe, nao wanalichukua Jina la Yesu Kristo.

<sup>391</sup> Basi, Baba, mwaga Roho Mtakatifu, wa Mafuta, juu yao, ili kwamba wawekwe katika huduma ya Bwana Mungu, ili wapate kuwa watenda kazi katika siku hii ya mwisho, ya uovu kwa maana tunatambua ya kwamba tuna wakati mdogo tu. Na Kanisa linaweza kuondoka wakati wo wote.

<sup>392</sup> Mwana-Kondoo anaweza, wakati wo wote, kuondoka kwenye madhabahu Kule juu, ama Kiti cha Enzi cha dhabihu, aje kutoka kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu ambapo dhabihu imewekwa, ndipo yote yamekwisha; hakuna matumaini tena kwa ajili ya ulimwengu; umekwisha. Ndipo unaingia katika misukosuko, ya mishindo ya matetemeko makubwa ya nchi, na—na mitikisiko mikuu kama ilivyokuwa wakati ule wa ufufuo. Na—na, ile—na ninii . . .

<sup>393</sup> Kama vile Kristo alivyofufuka kutoka kaburini wafu, wakati watakatifu watakapofufuka, jambo lile lile litatukia. Bwana, inaweza kuwa katika dakika yo yote. Tunaingojea siku hiyo yenye furaha kuwadia.

<sup>394</sup> Ulisema watoto Wako chini ya mikono Yako, Baba, sasa. Wavute wana-kondoo Wako kifua ni Mwako. Tujalie. Nawe uwalishe kwenye Neno, mpaka watakapopata nguvu kwa ajili ya utumishi. Tunawaweka Kwako sasa, Bwana. Jibu sala hii.

<sup>395</sup> Watwae ulisema, Baba, katika Marko, sura ya 11, “Mnapoomba, mkisimama na kusali, aminini kwamba mnayapokea mliyoomba, nayo yatakuwa yenu.”

<sup>396</sup> Na kwa moyo wangu wote ukiwa kwa Yeye ambaye amekuwa akiyafunua mambo haya kote katika miaka iliyopita, na Mihuri hii hapa katika juma hili lililopita; ninakuamini Wewe, Bwana Mungu, ya kwamba saa imewadia, imekaribia sasa, karibu zaidi kuliko tunavyowazia kweli, ya kule kuja Kwako.

<sup>397</sup> Ninakusihii ujibu sala yangu. Na naomba ujalie kila mtoto wa Mungu aliyelitwa, ambaye anaweza kusikia kutoka hapa, ama ye yote atakayefikiwa na kanda, naomba kwenye wakati huo . . . Ninawadai kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, juu ya msingi wa kujua hili ni Neno linalofunuliwa. Jalia Nuru ya jioni iangaze, Baba. Ninawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>398</sup> Sasa, wote, walio ndani ama nje, mnaoamini, na hamja—hamjajakiri mbele ya watu, ya kwamba mmeachana na dhambi; na u—unataka rehema za Mungu, na umezikubali katika Yesu Kristo. Kidimbwi . . . Wao watakuwa tayari kumbatiza mtu ye

yote anayetaka kubatizwa, leo ama kesho, sasa hivi ama wakati wo wote ule iwezekanapo.

<sup>399</sup> Mnaufurahia Muhuri wa Sita? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Unaona mahali ulipofunguliwa sasa? [“Amina.”] Umeuamini? [“Amina.”]

<sup>400</sup> Imesemwa, “Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta? Na mkono wa Bwana amefunuliwa nani?” Unaona? Amini habari hizo, ndipo mkono wa Bwana unafunuliwa. Mkono, Neno la Mungu, limefunuliwa.

<sup>401</sup> Bwana akipenda sasa, kesho asubuhi, nitajaribu niwezavyo kujibu maswali hayo. Nitatumia labda usiku uliosalia, na, ama karibu wote, katika maombi, juu yake. Nichukua kutoka kama saa moja mpaka masaa matatu kila usiku. Sikuingia kitandani jana usiku hata kidogo mpaka ilipokaribia saa saba, na kwenye saa tisa nilikuwa nikisoma. Unaona? Unaona?

<sup>402</sup> Nitawajibika kwa ajili ya jambo hili. Hiyo ni kweli. Tuko karibu sana kwa jambo lo lote, upuuzi wo wote, ama kubuniabunia mambo ko kote, ama kuamini nusu nusu. Sina budi kuliona jambo, kwanza. Na halafu, ninapoliona, halina budi kuwa katika Neno, pia. Na umbali huu, kwa neema ya Mungu, yameendana barabara. Nimeyachukua kutoka huko nyuma kabisa, mnajua hilo, na yame—yamechukuana vizuri kabisa.

<sup>403</sup> Halina budi kuwa BWANA ASEMA HIVI. Maana, si vile tu linavyosema kwa mimi kulijua, mimi mwenyewe, lakini Neno la Bwana ni BWANA ASEMA HIVI. Na hilo Neno ni hili hapa, nikichukua yale aliyonipa Yeye, na kuyaunganisha pamoja na kuwaonyesha. Kwa hiyo mnajua, ninyi wenyewe, ni BWANA ASEMA HIVI. Unaona?

<sup>404</sup> Hili hapa Neno, linasema hivyo. Na halafu ufunuo anaonipa Yeye, ambao ni kinyume cha yale ambayo ye yote wetu amewahi kuwazia; mbona, kinyume cha yale niliyowazia, maana sijapata kulifundisha namna hiyo. Lakini sasa, tunaona, linapatana vizuri kabisa. Basi ni kitu gani? Ni BWANA ASEMA HIVI. Unaona? Ni kweli kabisa. Imekuwa ni mahali palipofunguliwa, kushikilia pale, hata kwenye saa hii, ndipo Bwana anakuja na kulisukuma ndani moja kwa moja namna hiyo. Kwa hiyo, unaona, Hilo hapo. Ni, Hilo ni—ni Bwana. Loo!, nampenda! Ninampenda kwa moyo wangu wote.

<sup>405</sup> Sasa kumbuka, ninyi . . . Hatungeweza kwenda madhabahuni. Wengi waliinua mikono yao. Sasa, unaona, ni juu ya mtu binafsi, ni juu yako. Ni lo lote unalotaka kufanya. Unaona?

<sup>406</sup> Saa imekaribia sana, unapaswa kuwa ukijitahidi sana uwezavyo, si uvutwe. Unaona, kukazana tu, kukazana kuingia, “Bwana, usiniache nje. Usiniache nje, Bwana. Milango inafungwa; laiti ningaliweza tu kuingia ndani!” Unaona?

407 Mungu atafunga mlango siku moja. Alifanya hivyo katika siku za Nuhu, nao wakagonga mlango. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara kadha wa kadha—Mh.] Hiyo ni kweli? [Kusanyiko, “Amina.”]

408 Sasa kumbuka, Biblia ilisema, ya kwamba, “Katika zamu ya saba.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Wengine walilala katika zamu ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano, ya sita, ya saba. Lakini, katika zamu ya saba, kukatoka tangazo, kelele, “Bwana Arusi yuaja! Tokeni mkamlaki.”

409 Wale wanawali waliolala wakasema, “Aisee, ningetaka kupata Mafuta hayo kidogo sasa.”

410 Bibi-Arusi akasema, “Nina ya kutosha tu mahitaji yangu; nina ya kutosha tu. Kama unayataka, nenda ukaombe kwa bidii sana.”

411 Je! hammwoni yule mwanamwali aliyelala sasa? Waangalieni Waepiskopalia, Mpresbiteri, Mluteri, na kila kitu, wakijaribu kuyapata hivyo. Na shida yenyewe ni kwamba, badala ya kujaribu kumpata Roho Mtakatifu, wao wanajitahidi wanene kwa lugha.

412 Na wengi wao hunena kwa lugha, na wanaona aibu kuja kwenye kanisa hili kuombewa; wananitaka mimi niende nyumbani kwao nikawaombe. Unaita huyo ni Roho Mtakatifu? Huko ni kunena kwa lugha, lakini si Roho Mtakatifu. Unaona?

413 Sasa, ninaamini Roho Mtakatifu hunena kwa lugha. Mnajua ninaamini jambo hilo, mnaona. Lakini kuna mwigo Wake, pia. Naam, bwana. Ma—matunda ya Roho, ndiyo yanayothibitisha Hicho ni kitu gani. Matunda ya mti huthibitisha ni mti wa aina gani. Si lile ganda lake; tunda!

414 Sasa angalia, basi, wakati alipokuja, ile—ile saa ya mwisho. Na pale, walipoingia, ndipo wakaenda na kusema, “Vema, ninaamini ninaye sasa. Ninaamini ninaye. Naam, tunampata.”

415 A—a—afadhali nisiseme jambo hili, unaona, maana huenda likasababisha kuchanganyikiwa. Nilipo sema hivi majuzi, Kunyakuliwa, jinsi kungetukia, ni—ni- . . . Sasa, kama mkisema m—mtalistahimili, sawa. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Angalia. Angalia. Vema, hiyo ni juu yako.

416 Wakati yule mwanawali aliyelala, unaona, aliyedhani alikuwa ameomba vya kutosha, aliporudi, Bibi-arusi alikuwa tayari ameondoka. Kulipita, na hakujua habari zake; kama mwizi usiku. Ndipo wakaanza kugonga milango. Na ni kitu gani kilichotukia? Ni kitu gani kilichotukia? Wao walitupwa kwenye ule wakati wa Dhiki. Biblia ilisema, “Kutakuwa na kulia, na kuomboleza, na kusaga meno.” Hiyo ni kweli?

417 Kwamba ni wakati gani itakapotendeka, ndugu, dada, sijui. Lakini, mimi—mimi, mimi, huenda ikawa ni mimi tu hapa, sasa, unaona. Hili, hili ni ninii . . . Hili ni wazo langu. Unaona? Ni—ni—

ninaamini kumekaribia sana, mimi—mimi ni . . . Kila siku mimi—mimi ninataka . . . Ninajaribu tu kutembea kwa unyenyekevu niwezavyo. Unaona? Na sasa wakati, unajua, wakati ninii . . .

418 Jambo fulani lilitukia leo, nami niliona jambo fulani likija. Ni—nilininii tu . . . Sikuweza kupumua tena, unaona. Huyo hapo, amesimama pale, ile Nuru ndogo ikisimama moja kwa moja pale. Nayo ilikuwa iko hapa. Ninajua ni Kweli.

419 Nikawaza, “Ee Mungu, nisingeweza kusema jambo hilo. Si—siwezi kusema jambo hilo. Siwezi.” Nilitoka tu kwenye kile chumba, nikatoka nje, nikatembea huku na huko. Ndugu, nikawaza, “Jamani! Nifanyeje? Loo!” Unaona? Nami si—sina budi kwenda kuvua samaki, ama cho chote kile, ama mimi . . . Jamani, ungeninii . . . wewe . . . siwezi kuwaambia. Unaona?

420 Kwa hiyo tuna wakati mzuri. Sivyo? Bwana asifiwe! Amina! Unaona? Tuko katika—tuko katika wakati wa ajabu sana, unaona, kwa kuwa moyo wangu unafurika kwa baraka na furaha.

421 Lakini ninapowazia juu ya ulimwengu huu na maelfu ninaojua ya kwamba wamepotea, wamefunikwa na kivuli cheusi, a-ha, basi moyo wako unaugua tu. “Utafanya nini? Utafanya nini?” Unamsikia tu Roho Mtakatifu akilia, moyoni mwako. Kama vile hapana budi ilikuwa hivyo kwa Bwana wetu, wakati alipoutazama Yerusalemu, watu Wake Mwenyewe, unaona, akasema, “Yerusalemu, Yerusalemu, ni mara ngapi nimetaka kuwafunika kwa mabawa Yangu, kama vile kuku awafunikavyo pamoja vifaranga vyake, lakini hamkutaka.” Unahisi tu Roho Mtakatifu akisema, “Ni mara ngapi ningewakusanya, unaona, lakini hamkutaka.” Mnaona?

422 Tuko, tuko kabisa papa hapa kwenye jambo fulani, enyi marafiki. Hata iwe ni nini, Mungu anajua. Hakuna, hakuna mtu anayejua itakapotukia. Hiyo ni siri. Hakuna mtu anayejua itakapotukia.

423 Lakini Yesu alituambia, “Mtakapona mambo haya, mambo haya yote. Kama vile tu nilivyopitia, nikilinganisha na Muhuri wa Sita, na yale Yeye aliyosema katika Mathayo 24. Sasa kumbukeni aliyosema, “Mtakapona mambo haya yakija, kuanza kutimia, basi wakati uko mlangoni.” Angalia hasa aya ifuatayo, aya za 30—aya za 30 na ya 31 kama tulivyopitia huko nyuma, aya za 32, 33.

424 Yeye alisema, “Naye atawatuma Malaika Zake kwenye pembe nne za mbinguni, kwenye pepo nne, kuwakusanya Wateule Wake.” Hiyo ni kweli?

Kasema, “Sasa jifunzeni . . .”

425 Sasa kumbuka, Yeye alisimamia papo hapo. Yeye hakuendelea kamwe, baada ya Muhuri huo wa Sita. Yeye hakusema jambo lo lote kuhusu ule wa Saba. Yeye alitangaza wa

Kwanza, wa Pili, wa Tatu, wa Nne, wa Tano, na wa Sita. Lakini alisimama pale, yeye hakutaja cho chote juu Yake.

426 Angalia jambo lingine alilosema Yeye, “Sasa jifunzeni mfano.” Unaona? Ndipo anaanza na mfano. Yeye alisema, “Mambo haya yatakuwa.”

427 Yeye anawajibu hayo maswali matatu. “Ni lini . . . dalili hizi? Na ni nini dalili ya Kuja Kwako? Na ni nini dalili ya mwisho wa dunia?”

428 Na ule wa Sita, pale, ulikuwa ndio mwisho wa dunia. Na kule kupiga baragumu kwa malaika wa saba . . . “Akainua mikono, akaapa kwa Yeye aliye hai hata milele na milele, ya kwamba hakutakuwa na wakati baada ya haya.” Dunia inaza nyingine mpya. Imekwisha.

429 Nasi tuko hapa, papa hapa mlangoni. Loo! ninatetemeka. “Basi nifanye nini, Bwana? Ni—nifanye nini tena?” Unaona? Na, basi, wazia tu juu ya kuona mahali pale na hao watu wa thamani! Nilisimama pale, nikijiangalia mwenyewe. Nami nikawaza, “Ee Mungu, mbona, ha—hawawezi kukosa kitu hiki. Na—na—napaswa kuwasukuma. Ninapaswa kwenda kwenye kusanyiko na kuwashika, na kuwasukuma.” Huwezi kufanya hivyo. Uwe . . .

430 “Wala hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu.” Lakini hapa pana faraja moja tuliyo nayo, “Wote alionipa Baba watakuja.”

431 Lakini hao wengine, walio kwenye hayo madhehebu, wakiyategemea namna hiyo, unaona. “Naye aliwadanganya wote wale wakaa juu, walioishi juu ya nchi, ambao majina yao hayakuandikwa kwenye kile Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Loo! jamani! Kwa hiyo, unaona, ni jambo la huzuni.

432 Jambo pekee unaloweza kufanya ni ku—ku—ku—kudumu tu moja kwa moja na Neno. Angalia tu lo lote analosema ufanye, na basi ufanye hilo. Unaona? Lo lote analosema ufanye; fanya hilo.

433 Nawe unaangalia huko nje, na kusema, “Loo! jamani! Wao wanafanya jambo *hili*, halafu . . . Loo!” Ni ninii tu . . .

434 Hamtambui ni uzito wa jinsi gani! Sasa ninataka kusema jambo hili. Ninafikiri vinasasauti vimesimamishwa. Watu wengi sana husema, “Ndugu Branham, ukiwa na huduma ya namna hiyo . . .” (Sina budi kuwa mwangalifu, maana watu wanachukua tu kanda hizo na kujaribu kuzikosa kabisa, mnajua.) Kwa hiyo wakati wanaposema, “Ndugu Branham, laiti tungalikuwa na huduma,” hujui unalosema. Wewe, kweli, hujui yanayoambatana nayo, ndugu, dada. Loo! jamani! Na lile jukumu, wakati una watu wanaoshikilia yale unayosema! Kumbuka, kama ukiwaambia uwongo, Mungu ataitaka damu



yao mikononi mwako. Basi, wazia jambo hilo. Ni jambo la kuogofya sana.

<sup>435</sup> Kwa hiyo, uwe mtu mzuri. Mpende Yesu kwa moyo wako wote. Mfu- . . . Uwe mtu asiyejitakia makuu. Usija—usijaribu kamwe kuwazia jambo lo lote. Uwe asiyejitakie makuu, mbele za Mungu. Maana, jinsi unavyozidi kujitahidi kuwazia, ndivyo unavyoenda mbali Naye. Unaona? Wewe mwamini Yeye tu.

Wasema, “Sasa, vema, Yeye atakuja lini?”

<sup>436</sup> Kama akija leo, vema. Kama akija miaka ishirini tangu sasa, bado ni sawa. Mimi nitafanya tu jinsi ninavyofanya sasa, kumfuata Yeye. “Bwana, kama unaweza kunitumia mahali po pote, mimi hapa, Bwana.” Kama ni miaka mia moja kuanzia leo, kama vining’ina wa vining’ina wa vining’ina wa vining’ina vyangu wangali wataishi kuona jambo hilo likija, jalia. . . “Bwana, sijui itakuwa ni lini, lakini nijalie tu nienende vizuri leo, pamoja Nawe tu.” Unaona? Na—nataka. . . Maana, ni—nitafufuka siku hiyo, kama tu vile ningalishikwa na usingizi kidogo mahali fulani.

<sup>437</sup> Nikishuka kwenda kule, ile nyumba yenye fahari ya kifalme kule ng’ambo, ule Ufalme wa Mungu kule, ambako wote walio wazee watakuwa vijana, ambako nguo ndefu nyeupe ziko tayari! Hao wanaume na wanawake wamebadilika, katika uzuri, ule ustadi wa uzuri hasa wa—wa— wa mwanamume mwenye sura nzuri na—na mwanamke mwenye sura nzuri! Wakisimama pale katika uzuri wote wa kimo cha kijana mwanamke na kijana mwanamume, wakisimama pale! Wala hawawezi kamwe kuwa wazee, wala hawawezi kuwa wenye dhambi, wala hawawezi kuwa na cho chote cha kuonea wivu, wala chuki, wala cho chote kile! Loo! jamani!

<sup>438</sup> Nafikiri vinasasauti vimezimwa sasa. Nami—nami nina kama tu dakika tatu ama nne. Ninataka kuongea nanyi. Hilo ni sawa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa, hili ni jambo la kibinafsi tu, mnaona. Maana, kesho, na—na. . . Litakuwa ni jambo kubwa mno! Nafikiri ni afadhali niseme jambo hilo sasa, unaona, yale nitakayosema. Mimi. . . Hili ni kwa ajili yetu tu sasa. Nilikuwa nikinini tu. . .

<sup>439</sup> Mnajua, nina—nina mke ninayempenda, na huyo ni Meda. Na hata nisi—nisingemwoa, kwa sababu ya upendo wangu kwa mke wangu wa kwanza. Na hata hivyo, ingawa nilimpenda kiasi hicho, nisi—nisingemwoa kama Mungu asingeniambia nimwoe. Nanyi mnajua hadithi hiyo; jinsi alivyoenda kuomba, na jinsi nilivyoifanya. Na basi Yeye aliniambia hasa kile cha kufanya, na, “Nenda, ukamwoe,” na wakati hasa wa kufanya jambo hilo. Yeye ni mwanamke mzuri sana. Naye ananiombea usiku wa leo. Na kwa hiyo sasa ni saa mbili, huko nyumbani, labda yeye anaomba sasa.

440 Sasa angalia. Siku moja aliniambia, alisema, “Bill,” akasema, “ninataka tu kukuuliza swali kuhusu Mbinguni.”

Nikasema, “Vema, Meda, ni lipi?”

Akasema, “Unajua ninakupenda.”

441 Nami nikasema, “Ndiye.” Ilikuwa ni mara tu baada ya jambo hili kutukia hapa.

Akasema, “Unajua ya kwamba Hope naye alikupenda, pia.”

Nikasema, “Ndiye.”

442 Ndipo akasema, “Sasa,” akasema, “sidhani ningekuwa na wivu,” akasema, “lakini Hope alikuwa na wivu.” Kisha akasema, “Sasa, tutakapofika Mbinguni...Nawe ulisema ulimwona kule.”

443 Nikasema, “Yeye alikuwako kule. Nilimwona. Nimemwona mara mbili, kule.” Yeye yuko kule. Ananingojea mimi nje. Vivyo hivyo nani. . . Vivyo hivyo Sharon naye. Nilimwona, jinsi tu ninavyokuangalia wewe. Nilimwona kule. Ndipo nikasema. . .

444 Yeye akasema, “Vema, sasa, tutakapofika kule,” kasema, “ni nani atakayekuwa mke wako?”

445 Nikasema, “Nyote wawili. Hakuna ye yote atakuwa mke wangu, unaona, hata hivyo nyote wawili mnekuwa wake zangu.”

Akasema, “Siwezi kuelewa na jambo hilo.”

446 Nikasema, “Sasa, mpenzi, keti chini, hebu nikuelezee jambo fulani.” Nikasema, “Sasa, ninajua unanipenda, nawe unajua jinsi ninavyokupenda, na kwa upendo na heshima. Sasa, kwa mfano, vipi kama ningevaa nguo, nikaenda mjini; na maskini malaya fulani, mrembo sana, aje na kunikumbatia, na kusema, ‘Loo! Ndugu Branham, kwa kweli ninakupenda,’ aanze kunikumbatia na kunishikashika kimapenzi. Ungewazia nini?”

Akasema, “Sidhani ningependa jambo hilo sana.”

447 Nami nikasema, “Ninataka kukuuliza jambo fulani. Je! wewe. . .Unampenda nani zaidi ya wote, kama ingalikuwa ni kufikia shindano la kuamua, mimi ama Bwana Yesu?” Sasa, hayo ni mazungumzo tu, ya kifamilia.

448 Naye akasema, “Bwana Yesu.” Kasema, “Naam, Bill, ingawa ninakupenda, lakini, kabla sijamwacha Yeye, ningekuacha wewe.”

449 Nikasema, “Asante, mpenzi. Ninafurahi kukusikia ukisema jambo hilo sasa.” Nikasema, “Sasa, vipi kama maskini mwanamke yuyo huyo angemjia Yesu na kumkumbatia, aseme, ‘Yesu, nakupenda,’ ungewazaje juu ya jambo hilo?”

Akasema, “Ningefurahia jambo hilo.”

450 Unaona, inabadilika kutoka fileo kwenda wa agape. Unaona, ni Upendo wa hali ya juu zaidi. Unaona? Na hakuna

kitu kama mume na mke, kama...na kuzaa watoto. Yote yamekwisha, ji—jinsia ya kike na ya kiume. Zile tezi zote... Wao wote ni sawa, kule. Unaona? Hazipo hizo, tena. Unaona, hakuna, kabisa, tezi za jinsia. Unaona? Wewe ni ninii tu... Ndiyo, bwana. Jifikirie tu wewe mwenyewe bila tezi ya jinsia. Sababu ya kuwekewa hizo ndani yetu ilikuwa ni kwa ajili ya kuijaza nchi, unaona. Lakini, Kule, hakutakuwako na zo zote Kule. Hakutakuwa na tezi za kiume wala za kike. La.

<sup>451</sup> Lakini ustadi mkamilifu wa kazi ya mikono ya Mungu kitakuwako kule. Hiyo ni kweli kabisa. Lakini tutakuwa ni halisi kabisa. Hakuna—hakuna fileo, hata kidogo; wote ni agape. Unaona? Kwa hiyo, mke angekuwa si zaidi ya kitu fulani kinachopendeza ambacho ni—ni chako, naye...Ninyi ni mali ya mmoja kwa mwingine. Hakuna kitu kama...La, la, hakuna hata...Unaona, ile sehemu ya fileo hata haiko kule kamwe. Unaona, hakuwezi kuweko na kitu kama wivu; hakuna cha kuonea wivu. Hakuna kitu kama hicho kule. Hujui kamwe kitu kama hicho. Unaona? Na ni kijana mwanamume na kijana mwanamke mzuri tu, kuishi.

Halafu basi, baadaye, akasema, “Ninaliona jambo hilo sasa, Bill.”

Nikasema, “Naam.”

<sup>452</sup> Ninataka kuwaambia jambo fulani dogo lililotukia. Hii ilikuwa ni ndoto. Nilikuwa nimelala. Nami sijasimulia jambo hili hadharani hapo nyuma. Niliwaambia watu wachache, lakini sijalisema hadharani kamwe hapo nyuma, nijavyo mimi.

<sup>453</sup> Ni—niliota, yapata mwezi mmoja baada ya jambo hilo, ya kwamba nilikuwa nimesimama siku moja, nami nilikuwa nikiangalia ule wakati mkuu ambao...Si ile hukumu, sasa. Siamini Kanisa linakuja, (ninamaanisha, Bibi-arusi), anaenda hukumuni. Lakini, nilikuwa kule wakati taji zilipokuwa zikitolewa, unaona. Na kile Kiti ki—kikuu mno cha Enzi kiliwekwa *juu* hapa. Naye Yesu na yule Malaika anayeandika, na wengine wote, walikuwa wamesimama pale. Na kulikuwako na kitu kama vipandio vya orofa, vilivyoshuka namna *hii*, vya vipusa vyeupe; vikishuka chini, duara, ilifanyiza umbo la namna *hii*, kisha ikaendelea, hivi kwamba jeshi hili lote kuu lililosimama pale lingeweza kuona yale yaliyokuwa yanatukia.

<sup>454</sup> Nami ningesimama kule nyuma, kule nyuma kabisa upande mmoja. Na nilikuwa nimesimama tu pale, sina babari itanibidi kupanda vile vipandio. Nilikuwa nimesimama pale. Nilikuwa nimeona... .

<sup>455</sup> Yule Malaika anayeandika angeita jina fulani; nami ningejua, ningetambua jina hilo. Nikaangalia, na huko nyuma kabisa, hapa anakuja huyo ndugu, akitembea pamoja na dada fulani, wanakuja kwako, namna hiyo. Huyu Malaika anayeandika amesimama pale karibu na Kristo, (ni ndoto

tu sasa), na nilikuwa nikiangalia. Na majina yao yalikuwa mle ndani, yalipatikana katika Kitabu cha Uzima; Yeye angewaangalia, na kusema, “Ilikuwa—ilikuwa vema, mtumishi Wangu mwema na mwaminifu. Sasa ingia ndani.”

<sup>456</sup> Nikatazama nyuma, mahali walikokuwa wanaenda. Kulikuwako na ulimwengu mpya, na furaha kuu. Kisha akasema, “Ingieni katika furaha ya Bwana, ambayo—ambayo imekuwa yenu tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Unaona? Na, loo! nikawaza. . . Wao itawapasa kupitia pale, na kukutana wao kwa wao, na kufurahi tu, wakipanda milima na sehemu nzuri mno.

<sup>457</sup> Lakini nikafikiri, “Loo, hilo si ni jambo la ajabu! Utukufu! Haleluya!” Wakiruka-ruka tu!

<sup>458</sup> Kisha ningesikia jina lingine likiitwa. Ninawazia, “Loo! ninamjua huyo. Ninamjua. . . Ni- . . . Huyo, huyo hapo anaenda, pale.” Ninamwangukia namna hiyo.

“Ingia katika furaha ya Bwana, nanii Wangu mzuri na . . .”

“Loo!” ningesema, “Mungu asifiwe! Mungu asifiwe!”

Anasema tu, kwa mfano, kama vile waseme, “Orman Neville,” unaona.

<sup>459</sup> Na kisha ningesema, “Huyo ni maskini Ndugu Neville. Huyo hapo.” Unaona? Naye huyu hapa anakuja, kutoka kwenye umati wa watu, anapanda juu.

<sup>460</sup> Sasa anasema, “Ingia katika furaha ya Bwana, uliyowekewa tayari tangu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Ingia.” Na maskini Ndugu Neville anabadilika tu, na anaanzia huko nyuma, akipaza sauti tu na kupiga mayowe ya shangwe.

<sup>461</sup> Jamani, mimi ninapiga makelele ya furaha tu na kusema, “Mungu atukuzwe!” Nimesimama hapa peke yangu, nikiwa na wakati wa furaha sana, nikiwaangalia ndugu zangu wakiingia.

<sup>462</sup> Ndipo Malaika anayeandika akasimama pale, na kusema, “William Branham.”

<sup>463</sup> Sikuwazia kamwe ingenibidi kutembea nipande vipandio vile. Kwa hiyo basi niliogopa. Nikawazia, “Loo! jamani! Je! itanibidi kufanya jambo hilo?” Kwa hiyo nikaanza kutembea kwenenda kule. Na kila mtu tu akinipigapiga kwenye—kwenye. . . [Ndugu Branham anaonyesha kwa kujipigapiga mwenyewe mara nyingi—Mh.] “Ohaa! Ndugu Branham! Mungu akubariki, Ndugu Branham!” Wakinipigapiga nilipokuwa nikienda, kupita kwenye kundi kubwa mno la watu. Na wote wakinyosha mikono yao na kunipigapiga namna hiyo. [Ndugu Branham anaonyesha kwa kujipigapiga mara nyingi.] “Mungu akubariki, ndugu! Mungu akubariki, ndugu!”

<sup>464</sup> Nikawa nikienda. Nikasema, “Asanteni. Asanteni. Asanteni.” Kama vile mtu unatoka kwenye mkutano, ama cho chote kile, unajua.

465 Nami ilinibidi kutembea kwenye vile vipandio vikubwa mno vya vipusa. Nikaanza kwenda kupitia kule. Na mara tu nilipopiga hatua ya kwanza, nikasimama. Halafu nikawazia . . . Nikamwalia uso Wake. Nikawazia, “Ninataka kumwalia vizuri sana kwa upande huu.” Ndipo nikasimama.

466 Nilikuwa nimeweka mikono yangu namna *hii*. Nikahisi kitu fulani kimeingia mkononi mwangu *hapa*. Ulikuwa ni mkono wa mtu mwingine. Nikaangalia huku na huko, na pale alisimama Hope; hayo macho makubwa meusi, na hizo nywele nyeusi zimening’inia nyuma ya mgongo wake, amevaa nguo ndefu nyeupe; akiniangalia namna hiyo. Nikasema, “Hope!”

467 Nikasikia kitu fulani kikigusa mkono *huu*. Nikaangalia huku na huko, na huyo hapo Meda; hayo macho meusi yakiangalia juu, na zile nywele nyeusi zikining’inia chini, amevaa nguo ndefu nyeupe. Ndipo nikasema, “Meda!”

468 Nao wakaangaliana, unajua, namna hiyo. Walikuwa . . . Nimewashika mikononi mwangu, nasi hao tukaenda, tukielekea Nyumbani.

469 Nikaamka. Loo! nikaamka. Nami ni—nikaamka na kuketi kitini, na kulia, unajua. Nikawaza, “Ee Mungu, natumaini jambo hilo litatukia namna hiyo.” Wote wawili walikuwa na uhusiano nami katika maisha, na kuwazaa watoto, na mambo kama hayo; na sisi tuko hapa, tukitembea kuingia kwenye nchi mpya, loo! jamani, ambako ukamilifu na kila kitu. La, hakuna cho chote . . .

470 Loo! litakuwa ni jambo zuri mno! Usilikose. Usilikose. Kwa neema ya Mungu, fanya yote uwezayo kufanya, na hiyo itakuwa ni juu ya Mungu kushughulikia mengine basi.

Nampenda, nampenda  
Kwani alinipenda kwanza  
Na akanunua wokovu wangu.  
Mtini Kalvari . . .

471 Hebu na tuimbe tena, kwa moyo wetu wote. Sasa tuinue macho yetu kwa Mungu.

Nampenda

472 [Ndugu Branham anaondoka mimbarani na kumwomba mwanamke fulani, wakati kusanyiko linapoimba *Nampenda* mara nyingine tena—Mh.]

. . .mpenda  
Kwani alinipenda kwanza  
Na kununua wokovu wangu  
Mtini Kalvari.

473 Vema, sasa. Yeye hakutarajiwa kuishi hata mwisho wa mkutano huu. Hiyo ni kweli. Huyo hapo, mikono yote miwili hewani, akimsifu Mungu. Hiyo ndiyo sababu nilikuwa nikikawia hapa muda mrefu; bila kuwaambia ninalofanya. Nilikuwa nikizungumza juu ya Meda na hao wengine. Na kwamba

nilikuwa nikiangalia, kuona ni nini... Nilishikilia kuona ile Nuru ikizunguka huko na huko, kisha ikaenda ikaning'inia juu yake. Nikawaza, "Ndiyo hilo." Loo! hiyo si ni ajabu? [Kusanyiko linafurahi—Mh.]

Nampenda, nampenda  
Kwani alinipenda kwanza  
Na kununua wokovu wangu  
Mtini Kalvari.

<sup>474</sup> Sasa, huku mioyo yetu, [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda*—Mh.] wazia tu juu ya wema na rehema Zake.

... Nampenda (Amina!)  
... -penda kwa-..

<sup>475</sup> Sasa unaona jinsi ilivyo nafuu zaidi? Amina! Haya basi. Sasa...?...Nenda zako na uwe mzima. Amina! Neema ya Mungu imekutokea, kukufanya mzima. Amina.

... mtini Kalvari.

Loo, Mungu apewe utukufu!

Nampenda,...

Vema, mchungaji wenu.

Nam-...

<sup>476</sup> [Mtu fulani anasema, "Ndugu Branham, kesho unaanza saa tatu na nusu?"—Mh.] Kati ya saa tatu na saa tatu na nusu. Saa tatu, mahali fulani hapo. ["Baada ya kiamshakinywa? Saa tatu?"] Ninyi anzeni saa tatu. Mimi nitaanza saa tatu na nusu.



*UFUNUO WA MIHURI SABA*  
(The Revelation Of The Seven Seals)

Jumbe hizi za Ndugu William Marrion Branham zilihubiriwa kutoka tarehe 17 Machi mpaka tarehe 24 Machi, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, na Muhuri wa Saba ukaendelea tarehe 25 Machi katika Hoteli ya Sherwood. Baada ya kupata kanda za awali ambazo zinasikika vizuri na ni kamilifu zaidi, kitabu hiki kimechapishwa tena kwa mpangilio wa sasa. Kila jitihada imefanywa kuhamisha kwa usahihi Ujumbe wa sauti kutoka kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuuandika katika kitabu, na umechapishwa hapa bila kufupishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

Haki zote zimewekwa. Kitabu hiki hakiwezi kuuzwa, kuchapishwa tena, ama kufasiriwa katika lugha zingine, ama kutumiwa kwa kuchangisha fedha bila barua ya kuruhusia ya William Branham Evangelistic Association. Kilichapishwa tena katika mwaka wa 2006.

SWAHILI

©2001 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

**VOICE OF GOD RECORDINGS**  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)